SEPTEMBA MMXXIV-TOLEO LA XXXVI

# NGURUMO

*ya mwandishi*










## Miaka 3

Tumethubutu

Tumeweza


Tunasonga mbele










*Amata Ric*

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Miaka 3 tumethubu-tu… —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Gwamaka Mwamasage — Uk 03

**New In Town: —** MISHENI KHARTOUM, DUARANI— uk 04

**PITIO LA VITABU**— BIMA YA PEN-ZI—Uk 06

**MAKALA — SAIKOLOJIA**: ZIKUBA-LI CHANGAMOTO —Uk 06 na 07

**MAKALA:** Mjue 'BAYUME' **—**uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** IDD AMIN DADA— Uk 10

**Sako kwa Bako–** Wasemavyo wanav-itabu **—**Uk 11

**RIWAYA:** — SHAJARA YA MUUAJI '6'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '17'**-** Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '13- Uk 16

**HABARI:** Uzinduzi Kitabu cha SOKOINE – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Riwaya fupi kuliko zote —Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** THINK LIKE A CHAMPION —Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk20

**MALENGA WA KILEO:** Tumeanua Matanga & Mwateka Mwamtekea nani? — Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Maisha ni Mapambano '3'-Uk 23

**ELIMU JAMII:** — Ijue Monkey Pox (M POX) —Uk 24 na 25

**HADITHI:** Rais wa Chuo '3'— Uk. 26—29

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## TAHARIRI:
### TUMETHUBUTU, TUMEWEZA, TUNASONGA MBELE

Wasalaam,

Ni mwezi mwingine tena, jarida lako ulipendalo limekufikia. Hili sasa ni chapisho la 36 yaani linafunga ile miaka mitatu ya kuwapo mikononi mwako. Ni kama mchezo vile! Yaani kufumba na kufumbua.

Katika jarida hili tunachukua nafasi hii adhimu kukushukuruni nyote kabisa kwa jinsi mnavyotupeperusha mbali; ndani na nje ya Bara la Afrika. Leo hii tunajivuna kwa kuwa Ngurumo tunasomwa Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Afrika Kusini, Misri, Saudia, Marekani, Italia, Ujerumani na Norway. Nchi hizi nilizotaja ni zile tu ambazo ninapata mrejesho kutoka kwao lakini tunaamini kuwa zipo ambazo tunawafikia ila hatujasikia lolote kutoka kwao. Hii yote ni kazi yenu na tunakushukuruni sana kwa hili.

Ijapokuwa mwaka huu wa tatu tumeukamilisha kwa huzuni kubwa ya kuondokewa na mmoja wa wanangurumo (Rey Stanley) lakini hatuna budi kusonga mbele. Kazi ya Mungu haina makosa. Tunaamini kabisa kuwa popote alipo bado yupo nasi.

Nachelea kusema kuwa mpaka hapa tulipofikia ni kwa sababu ya kuamini na kutia nguvu katika jambo moja kubwa 'UTHUBUTU'. Mafanikio yoyote hayawezi kuja kama hautakuwa na UTHUBUTU. Jivike mabomu, jilipue, utaona matokeo. Tulipothubutu ndipo tukaona kumbe anhaaa twaweza. Basi ule moyo wa kuweza tukaufanyia kazi na leo hii tunawaambia kuwa 'tunasonga mbele'. Siku zote, mafanikio katika jambo lolote hufikiwa tu kwa kusimamia ndoto zako. Je unazo ndoto? Unatamani kuziishi ili ziwe kweli? Basi thubutu.

Pia nachukua nafasi hii pia kukushukuruni nyote mnaotoa michango mbalimbali ya machapisho kama makala, riwaya, mashairi na wale mnaokubali tufanye mahojiano na kuyaweka humu. Asanteni sana sana sana. Lakini ninapenda sana kuwaambia waandishi wa kazi za fasihi kuwa hili ni jarida lenu. Ukilitazama ni kama halina maana, ni kweli, lakini linakutangaza. Tuletee hadithi fupi, tutaiweka watu waburudike, una makala ya kifasihi tuletee tutaiweka watu wasome. Leo hii nakubembeleza utuletee 'content' amin amin nakuambia itafika wakati utatafuta nafasi hata ya kuandika jina lako kwenye hili jarida usipate.

Basi, tuendelee na mapambano yetu ya kila siku hususan katika ulingo huu wa fasihi ili mwisho wa siku tuifanye Tanzania yote iwe nchi ya kifasihi.

Asanteni na nakutakieni mwezi mwema!

*Richard Mwambe*
CEO

# MWANDISHI WETU:
## Gwamaka Mwamasage 'Maestro'

**Anaitwa Gwamaka Mwamasage. Gwamaka ni jina la Kinyakyusa lililobeba maana ya '-enye nguvu'. Lakini pia anajiita 'Maestro' kama Pen Name. Maestro ni neno la Kiitaliano lenye maana 'Bwana mkubwa (Master)'. Yeye ni mwandishi wa vitabu aliyepitia hustle nyingi sana katika kujitafuta. Ni mwandishi wa FATINA na USIKU WA DENI.**
**Isitoshe ni mtaalamu wa mifumo ya Kompyuta. Ni kijana asiye na nywele hata moja kichwani pake… katika toleo hili tunarudia tena mazungumzo yetu...**



Gwamaka Mwamasage 'Maestro'

Naitwa Gwamaka Mwamasage 'Maestro'

Nilianza kuandika riwaya miaka 15 iliyopita ambapo nilianza kwa kuandika hadithi magazetini, hadithi yangu ya kwanza ilitoka katika gazeti la Nipashe mwaka 2007 wakati huo nikiwa Kyela, mkoani Mbeya ambako ndio nyumbani kwetu.

Niliandika kwa miaka miwili mfululizo kabla mwaka 2009 sijahamia mkoani Njombe wilaya ya Makete wakati huo ikiwa ndani ya mkoa wa Iringa hivyo sababu za kimazingira na changamoto mbalimbali za kimaisha zikanitupa nje ya ulingo kwa muda mrefu kabla sijaamsha ari mwaka 2021 nilipoamua kuandika riwaya kwa kuandaa kitabu moja kwa moja ambapo nilichapa toleo la kwanza la simulizi ya FATINAH ikiwa na sehemu ya kwanza tu.

Kilichonisukuma kuandika riwaya, kwanza mimi nimekuzwa katika mazingira ya kusoma. Baba yangu ni mwalimu mstaafu sasa, hivyo maisha yangu yote nimekuzwa katika mazingira ya kuona na kusoma vitabu mbalimbali. Pili, nimerithi hiki kipawa kwa wazazi wangu wote wawili ambapo baba yangu naye alikuwa/ ni msanii kiasili, ukiacha masomo aliyokuwa akifundisha kuwa ya sanaa lakini wakati wote wa makuzi yangu nimemshuhudia akifanya kazi mbalimbali za sanaaa ikiwamo kuchora na uandishi akijikita zaidi katika uandishi wa mashairi, mama yangu naye ni msomaji mkubwa sana. Tatu, ni kipawa kilichochagizwa na hayo mambo mawili kupelekea kuchochea ari ndani yangu ya kusoma na kuandika.

Changamoto ninazokutana nazo ni za kimazingira zaidi maana naishi 'mkoani' na shughuli zote zinafanyika jijini Dar, hapa ndipo simu inapochukua majukumu mazito kuhakikisha kila jambo linakwenda sawa. Nashukuru utandawazi umerahisisha mambo kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa. Zingine bado sijakutana nazo nazisikia tu kwa watu, ni kwa bahati nzuri napata ushirikiano wa kutosha kwa kila aliye ndani ya tasnia nawashukuru mno waandishi na wasomaji wote pamoja na ugeni wangu.

Mpaka sasa nina kitabu kimoja **(kwa sasa ana vitabu viwili)** tu sokoni ukiachilia mbali vile ambavyo bado viko jikoni.

Nawashauri watanzania wapende kusoma, haijalishi unasoma nini lakini kuna maarifa mengi na makubwa ndani ya vitabu. Ukiwaweka katika uzani sawa msomaji na asiye msomaji iko wazi kwamba anayesoma ana maarifa, ufahamu na utambuzi binafsi kuliko yule asiyesoma.

Mimi huwa naamini mtu anayesoma anatosha kabisa kujiita msomi kuliko yule mwenye vyeti vya kitaaluma, elimu ya

Darasani, hiyo ni ziada katika maisha.

Malengo yangu ni kuacha alama katika uga wa fasihi andishi, natamani siku moja nisaidie waandishi wanaochipukia kama ambavyo waandishi wengine wananishika mkono hivi sasa.

Mwisho, lakini kwa umuhimu naomba watanzania wanipokee, kutimia kwa ndoto yangu ndio kutimia kwa ndoto za vijana wengine ambao wanatamani kuandika lakini hawana pa kuanzia, narudia tena nawashukuru sana waandishi na wasomaji wote kwa moyo wao. Asante.

Waweza pata vitabu vyake kwenye maduka kama Kona ya Riwaya, Posta Mpya kwa Joji jijini Dar',

Gwamaka Mwamasage,
Njombe,
Tanzania.

## NEW IN TOWN :
## MISHENI KHARTOUM, DUARANI

**MISHENI KHARTOUM 01**
**(Kufa ama kupona)**
**Na. Abubakar Nkundwason**

Kachero Othuman Seyunguson kutoka nchini Tanzania, anatumwa kwenye misheni ya kuinusuru Ikulu ya taifa la Sudan ambayo ilikuwa inanyemelewa na wadhalimu.

Misheni hii iliyopewa jina la Misheni Khartoum 01, haikuwa misheni ya kitoto. Ni misheni iliyojaa usaliti wa kila aina, lakini zaidi adui mkubwa wa taifa hilo la Sudan Brigedia Omar Al Bashir alikuwa amejipanga kwelikweli na aliihitaji Ikulu ya taifa hilo la Sudan kufa na kupona.

Kachero Seyunguson akiwa pamoja na msaidizi wake, Farida, mwanadada kutoka nchini Kenya, aliyepikwa akapikika kwenye mambo ya mapambano ni kana kwamba walitolewa sadaka kwenye misheni hii maana kila aliyekutana naye mbele yao hata yule waliyedhani yupo upande wao, alikuwa ni adui.
Je nini itakuwa hatima ya wawili hawa kwenye misheni hii iliyojaa visa na mikasa ya kuburudisha, kuelimishaa na kuacha kinywa wazi?

Ungana na mwandishi Abubakar A. Nkundwason, katika riwaya hii ya aina yake.

**Hii ni NEW IN TOWN… jikamatie nakala yako sasa pale duka la vitabu**
**KONA YA RIWAYA kwa Tsh 8000 tu. Au wasiliana na Zamira Sanguti 0655428085**

**DUARANI**
**Na. Amosi Bwire**

Maisha ya Sophia yanaingia kwenye mtafaruku usio kifani baada ya mpenzi wa zamani wa Tuntu, mumewe, kuzuka kwa kisasi kikali kinachozua mlolongo wa matukio ya kutisha, yanayoisambaratisha ndoa yao.

Katikati ya kizungumkuti hicho, Tuntu anafanya mauaji, yanayompelekea kukwapua mamilioni ya pesa za mwajiri wake na kutoweka kusikojulikana, akimwacha Sophia akabiliawe na athari za udhalimu wake.

Miaka miwili baadae, anapoibuka na kumkuta Sophia mikononi mwa mwajiri aliyemwibia, mipaka kati ya wema na uovu inafutika, uadui mkubwa unafufuka, siri nzito zinafichuka na kupelekea dhoruba ya machozi, jasho na damu iwaviringe duarani na kuwatosa kwenye kilindi cha maangamizi.

Kwenye sakata hili la kusisimua, lililojaa misukosuko ya mahaba, uovu uliokithiri, majeraha ya chuki na visasi vya kutisha nani atasalia imani inapotoweka na kweli inapoanikwa hadharani?

DUARANI ni janga. Ni hadithi ya maisha yaliyopoteza mwekeo. Ni ndoa iliyovunjika vibaya kiasi kwamba mnapojaribu kuunganisha vipande, mnakutana na msiba mkubwa.

Huu ni mkono wa Amos Bwire au mwite Baba BM



***Pata nakala yako sasa kwa shilingi 10,000 tu, Piga Simu Namba 0672132218 kwa maongezi, SMS au whatsApp. Offer hii ni hadi Oktoba 15, 2024.**

# KITABU: BIMA YA PENZI

**BIMA YA PENZI UTUNZI WA MWANDISHI**

**GOIMA MWAMWINGILA.**

**Mchambuzi: Neema Mgao**

Habari ya kuamka mpenzi rafiki yangu! Bila shaka u salama na ikiwa umeamka na changamoto yoyote ni matumaini yangu kuwa changamoto hiyo itapita, ila itapitaje? ni wewe kwanza kuikubali kisha ukaishughulikia huku ukiwa umemkabidhi Maulana changamoto hiyo ili akupe njia za ufumbuzi. Nakuombea heri, najiombea na mimi pia.

Leo nimewiwa kufanya uchambuzi kidogo. Nitachambua kitabu hiki kilichopokelewa vizuri sana na jamii kwa ujumla. Nacho ni BIMA YA PENZI.

Kama tujuavyo, dunia imeshatambulishwa BIMA nyingi sana; kuna BIMA YA AFYA, BIMA YA GARI, BIMA YA NYUMBA, BIMA YA BIASHARA n.k. Lakini niwe muwazi kwamba ni mara yangu ya kwanza kusikia BIMA YA PENZI. Eti, wewe mwenzangu uliwahi kusikia wapi kuwa kuna mahali ipo BIMA YA PENZI watu wanakatia bima mapenzi yao? Sina shaka kuwa umenijibu haujawahi. Sasa mwandishi GOIMA MWAMWINGILA anataka kusema nini na jamii kuhusu BIMA YA PENZI?

BIMA YA PENZI ni kitabu nilichobahatika kukipata mwishoni mwishoni mwa mwezi Mei, ni kitabu kilichosheheni kurasa 325 zilizo na ujazo haswa, ubora wa kitabu kuanzia jalada, kurasa, mpangilio wa maandishi, haumfanyi msomaji kujutia kusoma wala kununua nakala hii.

BIMA YA PENZI kimetolewa kwa kiwango kikubwa sana, na ni kitabu kinachotunzika. Kwa ubora huu kitaka sana, ni utunzaji wako tu.

**UJUMBE ULIOPO NDANI YA KITABU BIMA YA PENZI.**

Mwandishi anatupa jumbe nyingi sana humu ndani, lakini dhima kuu au ujumbe mkuu ni kuhusiana na MAPENZI na NDOA. Mwandishi ameyaangazia mapenzi kwa namna ya ajabu sana, ipo sauti ndani ya mwandiko wake nilikua nikiipata katika fahamu zangu, hasa alipokua akidadavua mambo fulani fulani yahusuyo maisha, mapenzi, biashara, maradhi hasa ya Saikolojia, chuki, husda, na mengineyo mengi.

Kitabu hiki kimebeba elimu kubwa sana katika nyanja nyingi,.

### Chuki

Nilipokua nasoma, nikagundua mwandishi ameongea kitu nyeti sana, chuki ndani ya familia. Tunawaona ndugu zake GAUDENSI MAKUNJA wakiibua chuki dhidi ya mdogo wao, kumpiga vita katika biashara na hata vita katika mambo yake mbali mbali hasa ya kimahusiano, kwani tunaona jinsi walivyoshirikiana na ASHA msaidizi wa GAUDENSI katika kusuka njama na mwanadada mwanamitindo kutokea nchini MADAGASCAR bibie MAGGIE BELL. Kitu ambacho wanafanikiwa kuwatenganisha kwa muda wapendanao hawa. Madhara ya chuki zao ndugu hawa inapelekea si tuu kumpotezea mwelekeo mdogo wao bali pia kuipotezea mwelekeo familia nzima kwa kukwamisha biashara ya familia yao. CHUKI HAIFAI, CHUKI

**PITIO LA VITABU**




INA MADHARA MAKUBWA SAANA. TUPENDANE.

**BIMA YA PENZI**

Pamoja na jumbe zote lakini hebu tujikite katika lengo halisi la kitabu hiki. Mwandishi anataka kusema nini?

GAUDENSI na LUCIA ni wahusika ambao mwandishi amewaumba kuwa ndio wahusika wakuu katika riwaya yetu hii. Wasifu wao na shughuli zao ni kama zilivyoainishwa kwenye kitabu, GAUDENSI ni mtaalamu wa biashara huku LUCIA ni mtaalamu wa mambo ya Saikolojia. Wahusika hawa wanafanikiwa kufunga ndoa, ndoa yenye baraka kwa pande zote mbili. Kila kitu kinawekwa wazi, kasoro kitu kimoja tuu, BIMA YA PENZI.

***Itaendelea toleo lijalo***

# -SAIKOLOJIA-
## ZIKUBALI CHANGAMOTO

**Madam Neema Mbilinyi Mgao**
**Simu: 0746 139 654**
**Whatsapp: 0746 139 654**
**Dodoma.**



Uhali gani ndugu na rafiki yangu, sina shaka unaendelea vyema kabisa katika shughuli zako za kila siku. Nikukaribishe katika kukisoma kitabu nilichokiandika nikilenga kuitibu jamii katika mambo mbalimbali yahusuyo SAIKOLOJIA.

Kitabu nimekipa anwani JITIBIE KISAIKOLOJIA nikilenga kukujengea uwezo wa kujitibu masahibu yako ya kila siku kabla haujamtafuta MWANA-SAIKOLOJIA akutibu au kukushauri jambo lako.

Baada ya kukueleza hilo basi sambamba na maudhui ya kitabu hicho,leo nikueleze na kukupa tiba mojawapo ya KISAIKOLOJIA. Naita 'tiba' na pia ni kinga maana ukiiweza hii basi nina uhakika hautoteteleka pindi ukutwapo na changamoto au tatizo.

Maisha ya kila siku ya mwanadamu yamezungukwa na mambo mazuri na mabaya. Yaani maisha yangu ya kila siku ni eidha yaanze na kumalizika kwa ubaya, au yaanze na kumalizika kwa uzuri, na sio ajabu pia yakaanza kwa uzuri na kumalizika kwa ubaya, pia usishangae yakaanza kwa ubaya na kumalizika kwa uzuri. YOTE YANAWEZEKANA.

Maisha ya kila siku hutegemeana na siku yako umeipangiliaje, kwamba wewe unapanga kwanza ndipo Mungu nae anaweka uwepesi wa mipango yako. Kitaalamu, ubongo wa mwanadamu pindi tu anapoamka huwa upo wazi, [upo fresh], pindi pale mtu anapotoka usingizini ubongo huwa hauna kitu ila kadri mtu anavyoanza kukumbuka mambo ya nyuma ndio anaujaza upya ubongo huo, kwa maana pale mtu anapolala na kila kitu katika ubongo wake huzimika sawa na SWITCH ya umeme, kwamba ukiwasha ndio unapata matokeo chanya na ukiizima basi kila kitu kinasimama utekelezwaji wake.

Mungu amemuumba kila mwanadamu kuwa na akili yake. Kila jambo linapotokea ni lazima binadamu kutumia akili, lakini changamoto inapotokea mwanadamu hushauriwa kutumia akili na busara pamoja katika kuitatua changamoto hiyo.

AKILI NI NINI?.
Akili inatafsirika kuwa ni ile hali ya kutatua changamoto. Mfano; unatembea njiani, ghafra mvua ikaanza kunyesha, unapoamua kusimama mahali ambapo mvua haifiki au unapoamua kununua mwamvuli, hapo umetumia akili katika kutafuta suluhisho la tatizo lililokukumba.

BUSARA NI NINI?.
Busara inatafsiriwa kama ni ile hali ya kujiandaa katika kupambana na changamoto kabla haijatokea. Mfano; Unatoka nyumbani, ukaona dalili ya mvua juu angani na ukaamua aidha kusitisha safari au ukabeba mwamvuli ili kujiandaa na kujikinga na mvua ikiwa itakukutia njiani katika safari yako. Hiyo ni busara.

Leo tunazungumzia kuzikubali changamoto. Nachelea kusema kuwa, bila kukutana na changamoto basi yawezekana wewe ni mfu. Kila aliye hai ni lazima kukumbwa na changamoto za hapa na pale. Uwezo wako wa kuchanganua changamoto zile unazokutana nazo, uwe mkubwa wa kushughulikia changamoto zinazokukumba. Hapo huwa imara pale unapokua unakumbwa na mitihani ya hapa na pale. Yaani kadri unavyokutana na kupokea changamoto inakupa wepesi wa kushughulikia changamoto zako.

Uwezo wako wa kushughulikia matatizo yako huwa imara zaidi pale unapokabiliana na changamoto hizo. Zikubali changamoto kwa namna na maana kubwa ya kutafsirika kuwa hata usipozipokea ndio jambo limeshatokea hivyo huna budi kulishughulikia. Zikubali changamoto ili usiumize fikra na saikolojia yako. Watu wengi wanakumbwa na sonona katika mambo mbali mbali kwa kushindwa kupokea huo wakati wa changamoto unapomkuta.

Leo jiulize mpendwa rafiki yangu, akili yako umeiandaa kukabiliana na changamoto yako? Busara yako katika kujiandaa na kukumbana na changamoto mbalimbali zinapokukumba ipo kwa kiwango gani? Bus-

# -SAIKOLOJIA–
# ZIKUBALI CHANGAMOTO

ara yako umeiandaa kuwa hata ukimfumania mke au mume wako au mpenzi wako, kuwa utamsamehe hautomdhuru? Au ndio wewe ambae utaenda kuvaa sare za njano katika MAGEREZA YA ISANGA PALE DODOMA-TANZANIA? Kwamba akili yako ina uwezo wa kukabiliana na yale maumivu ya kuachwa na usimdhuru yule anaekuacha?.

Kuwa tofauti, kubali kupokea changamoto hizo na nyingine zozote utakazokutana nazo. Kwamba watu wakuone kuwa uko tofauti, alimradi ni mfuasi wa Makala zangu nikuwekeazo kila mwezi, basi nitafurahi ukapokea na kunipa matokeo chanya kuwa kile nachokiandika kila iitwapo mwezi mpya, na hata sasa nimekutolea kitabu JITIBIE KISAIKOLOJIA nitafurahi nikiona kile nachoandika kikakufaa na ukaishi nacho.

Furaha yangu itakua katika kiwango kikubwa zaidi pale ambapo kila unaposoma unabadilika na kubadilisha pia jamii ikuzungukayo.

ZIKUBALI CHANGAMOTO ILI UPATE NA KUKUZA AKILI NA BUSARA KATIKA KUZITATUA.

ASANTE.

**THE MAGIC AUTHOR.**
**MADAME NEEMA MGAO.**
**0763013206**

**Kutoka katika dawati la mhariri**
Tunamshukuru sana Madam Neema Mgao 'The Magic Author' kwa makala zake za Saikolojia kwa matoleo yote ya mwaka huu wa tatu wa jarida hili la Ngurumo ya Mwandishi.

Shuhuda nyingi zimemfikia na kutufikia kuhusu namna ambavyo makala hizi za saikolojia zimesaidia wasomaji wetu mbalimbali kuweza kujitibu na kuwa sawa katika harakati za kimaisha.

Labda kwa kifupi tu nikuwekee anwani za makala zote alizotoa katika mwaka huu wa tatu (3) wa Ngurumo ya Mwandishi, ili kama utahitaji zilizotoka nyuma basi tutakupatia jarida husika.

Oktoba 2023 - HAKUNA ULICHOPOTEZA
Novemba 2023 - UWE NA KITU CHA KUJIRINGIA
Desemba 2023 - UWE NA KITU CHA KUJIRINGIA
Januari 2024 - USIWE CHANZO CHA MATATIZO YAKO
Februari - USIJITOTOSHE ILA USIACHE KUWA MNYEMYEKEVU
Machi - WAZA MAWAZO CHANYA
Aprili - SAIKOLOJIA YA MAPENZI
Mei - TAFUTA UPEKEE WAKO, RINGIA NA UUTUNZE HUO
Juni - ITUNZE NGUVU YA ASILI
Julai - USIMWACHIE NAFASI
Agosti - SAIKOLOJIA YA MALEZI
Septemba - ZIKUBALI CHANGAMOTO

Lakini wakati tunapokamilisha mwaka huu wa tatu wa Ngurumo ya Mwandishi, Mwanasaikolojia wetu, Neema Mgao ametuletea kitabu chenye anwani JITIBIE KISAIKOLOJIA.


Kitabu hiki kilichoingia sokoni mwishoni mwa mwezi wa Septemba kinaudhihirisha umahiri wa Neema Mgao katika uga wa Saikolojia. Ni msaada mkubwa kwa wote wanaougua maradhi yanayotokana na kuathiriwa kisaikolojia.

Hakikisha unakamata nakala yako mapema sana ili uweze kujitibu kwa njia hii. 'Maarifa mengi yamefichwa kitabuni'.

Kitabu hiki kinapaikana kwa bei ya Tsh 10,000 tu. Wasiliana naye kupitia no. +255 763 013 206 ili akupatie copy yako.

**Pia kinapatikana**
**Dodoma - 0763013206**
**Dar es salaam -**
- **Kijogoo Book Shop Kariakoo 0678683278**
- **Kalamu Tulivu Magomeni 0718975659**

**Makambako**
**APM Bookshop**
**0674246969**



# 'BAYUME' MOHAMED HUSSEIN
## MWALIMU WA KISWAHILI NA MCHEZA SINEMA ALIYEUAWA KWENYE KAMBI YA MATESO YA HITLER

**Bayume Mohamed Husen (jina la kuzaliwa: Mahjub bin Adam Mohamed)**

Alipokuwa akifanya utafiti katika Hifadhi ya Taifa ya Ujerumani, Bi. Marianne Bechhaus- Gerst alikutana na hati inayoonesha kulikuwa na mwalimu wa Kiswahili anayeitwa Bayume Mohamed Husen (jina la kuzaliwa: Mahjub bin Adam Mohamed) ambaye alipelekwa kwenye kambi ya mateso ya wa NAZI ya Sachsenhausen huko Oranienburg, Kaskazini mwa Berlin enzi zaUtawala wa Hitler.

Jambo hili lilimfanya Bi. Marianne achunguze zaidi hadithi ya Bayume na kuandika kitabu **Treu bis in den Tod: Von Deutsch-Ostafrika nach Sachsenhausen – Eine Lebensgeschichte (Mwaminifu hadi Mauti : Kutoka Koloni la Ujerumani la Afrika Mashariki (Tanganyika) hadi Sachsenhausen**

**Hadithi ya Maisha ya Bayume.**

Bayume Mohamed Hussen alizaliwa mwaka wa 1904 mjini Dar es Salaam mtaa wa Kaiserstraße (Kaiser Street/ Br. ya Sokoine) wakati huo jiji lilikuwa sehemu ya Koloni la Ujerumani lililojumuisha Tanganyika (sasa Tanzania), Rwanda na Burundi. Bayume alikuwa askari (mpagazi) na mwigizaji wa filamu.

Baba yake alikuja kutoka Sudan (inasadikika alikuwa ni Mnubi) na alikuwa askari kwenye jeshi la kikoloni la Ujerumani.

Vita vya Kwanza vya Dunia vilipoanza mwaka 1914, Bayume akiwa na umri wa miaka 10 tu alijiunga na baba yake kufanya kazi kama askari mtoto katika jeshi la kikoloni la Ujerumani. Kulingana na kitabu cha Bi. Bechhaus-Gerst, askari wengi watoto walikuwa wakifanya kazi kama "watoa ishara na wapagazi" wakati wa vita na hilo ndilo jukumu ambalo Bayume alilokuwa anafanya kwenye jeshi la kikoloni la Ujerumani. Baba yake alifariki kwenye hii vita na pia Bayume alijeruhiwa.

Baada ya Vita ya Dunia I kuisha, mwaka 1925 Bayume alifanya kazi kwa muda Zanzibar akiwa mwalimu na mhudumu kwenye meli ya kijerumani iitwayo Woermann Line Shipping Line.

Mnamo 1929, Bayume aliamua kuacha kazi yake katika meli na kwenda Berlin kudai mafao yake ambayo alikuwa hajalipwa yeye na baba yake wakati wakiwa askari kwenye jeshi la Ujerumani. Ombi lake lilikataliwa na Ofisi ya Mambo ya Nje. Baada ya hapo Ujerumani walijaribu kumrudisha Afrika ila Bayume alipinga na badala yake akaishia kundelea kuishi Berlin kimazabe.

Akiwa Berlin, Bayume alifanya kazi kama mhudumu katika baa ya "Wild West Bar" (Haus Vaterland) huko Potsdamer Platz kuanzia 1930 hadi kufukuzwa kwake mnamo 1935. Wakati huo huo pia alikuwa akifanya kazi katika "Idara ya Masomo ya Kigeni," kwenye Chuo Kikuu cha Berlin (Chuo Kikuu cha Friedrich Wilhelm) kama mwalimu/msaidizi wa Lugha ya Kiswahili (kati ya 1931 na 1941). Mnamo mwaka 1941 aliacha kazi yake katika chuo kikuu, kwa sababu ya kunyanyaswa na kufedheheshwa na maprofesa wa kizungu.

Mwaka 1933, siku tatu kabla ya kuteuliwa kwa Hitler kuwa Kiongozi wa Ujerumani, alimuoa Mary Schwandner na walizaa mtoto wa kiume (Ahmed Adam Mohamed Husen) na binti (Anne Marie Husen), aliyezaliwa mwaka 1936. Watoto wote wawili walikufa wakati wa utoto (Ahmed mwaka 1938 akiwa na umri wa miaka 5, Anne Marie mwaka 1939 akiwa na umri wa miaka 3). Mwaka huo huo, Ba-



yume alipata mtoto mwingine na mwanamke mwingine wa kiJerumani- Lotta Holzkamp ambaye alizaa nae mtoto wa kiume (Heinz Bodo Husen). Heinz Bodo alikuja kufariki akiwa na miaka 11 tu wakati Mji wa Berlin uliposhambuliwa kwa mabomu mwaka 1945.



Kazi nyingine aliyokuwa anaifanya Bayume iliyompa umaarufu ilikuwa ni uigizaji wa filamu na kazi hii aliifanya mwaka 1934 hadi 1941 na alikuwa ameigiza katika filamu zisizopungua 23 za kijerumani na filamu ya kwanza ilikuwa inaitwa "Die Reiter von Deutsch-Ostafrika (The Riders of German East Africa)



**'Bayume' katika moja na mbili**

na katika filamu ya "To New Shores" ya mwaka 1937 aliigiza pamoja na waigizaji wakuu kama ziada.

Wakati wa utengenezaji wa filamu ya Die Reiter von Deutsch-Ostafrika (The Riders of German East Africa), Bayume alifanikiwa kurudi Tanganyika kwa muda mfupi.

Filamu ya mwisho kuigiza ilikuwa kati ya 1940- 41 iliyokuwa filamu ya propaganda ya waNAZI, iliyoitwa "Carl Peters" na aliigiza kama Ramadhani akiwa mkalimani na msaidizi wa Carl Peters.

Mwaka 1941 wakati wa utengenezaji wa filamu ya "Carl Peters" Bayume alianza uhusiano wa kimapenzi na mwanamke wa kizungu wa Kijerumani. kitendo hiki kilimuingiza kwenye matatizo mkubwa ambayo yalimfikisha kwenye kambi ya mateso (concentration camp) ya Sachsenhausen baada ya kukamatwa.

Baada ya kulaaniwa alianza kuchunguzwa na alikamatwa na maGestapo na kwa shitaka la unajisi wa rangi na kufungwa/ kupelekwa kwenye gereza la Gestapo maarufu huko Alexanderplatz 1 bila kesi. Wakati huu (wa uongozi wa Hitler) ilikuwa marufuku kwa weusi kufanya tendo la ngono na "wanawake wa kizungu".

Baada ya kufungwa kwa miaka 3 kwenye kambi ya mateso, mnamo mwaka1944, Bayume alifariki kutokana na hali mbaya gerezani.

Mpaka mwaka 1990 hatima ya Bayume Mohamed Husens nchini Ujerumani ilikuwa haijulikani. Kutolewa kwa kitabu chake na Bi. Marianne Bechhaus-Gerst mwaka 2007 kilihamasisha watu kuanza kufuatiliwa maisha yake. Mnamo 1999, Chuo Kikuu cha Humboldt huko Berlin kilitoa Hotuba ya Bayume, ambayo ilifunguliwa na kuwasilishwa wa mwanahistoria wa Kenya Atieno Odhiambo.

Pia kuna jiwe la kaburi lenye maandishi "Mohamed Husen" liko kwenye makaburi ya vita huko Freiheitsweg, Berlin.

**Kitabu kinachoelezea maisha yake**




Mwaka 1999 Bayume aliwekwa historia nchini Ujerumani kwa kuwa mtu wa kwanza mweusi kupewa kumbukumbu kama mwathirika wa mauaji ya Utawala wa Hitler (Third Reich). Pia kuna Jiwe la ukumbusho la Stolperstein lililoko mbele ya makazi yake ya zamani pale 193 Brunnenstraße, Berlin.

~ Kutoka kwenye kitabu cha Marianne Bechhaus-Gerst. 2007

**Kaburi la Mahjub Bin Adam Mohamed (Bayume)**



# IDD AMIN DADA

**KATIKA watu ambao wamewahi kushika nyadhifa kubwa na za juu katika nchi za Afrika, kamwe hatutoweza kumsahau huyu IDD AMIN DADA. Yeye alikuwa zaidi ya rais. Ungana na mwandishi wetu wa makala haya akujuze.**

Idi Amin Dada alikuwa rais wa Uganda kuanzia mwaka 1971 hadi 1979, akijulikana kama mmoja wa viongozi wa kidikteta na wenye ukandamizaji barani Afrika. Alizaliwa mnamo mwaka 1925 huko Koboko, Kaskazini-magharibi mwa Uganda, katika kabila la Kakwa. Hata hivyo, tarehe halisi ya kuzaliwa kwake haijulikani vizuri.



**Uchimbuzi na Kazi za Awali**

Amin alijiunga na jeshi la kikoloni la Uingereza la *King's African Rifles* (KAR) mnamo mwaka 1946. Alipanda vyeo haraka kutokana na umahiri wake wa kijeshi na ushiriki wake kwenye kampeni mbalimbali, kama ile ya Kenya dhidi ya Mau Mau na Burma. Alipata umaarufu kutokana na nguvu zake za mwili na ujasiri wa kivita.

**Kupanda Madarakani:**

Baada ya uhuru wa Uganda kutoka kwa Uingereza mnamo mwaka 1962, Amin aliendelea kupanda vyeo katika jeshi la taifa. Mnamo Januari 25, 1971, alifanya mapinduzi ya kijeshi dhidi ya rais Milton Obote wakati akiwa nje ya nchi kwa mkutano. Amin alitwaa madaraka na kutangaza kuwa yeye ndiye rais wa Uganda.

**Utawala Wake**

Utawala wa Idi Amin ulitawaliwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, mauaji ya wapinzani, mateso, na vitendo vya udhalilishaji. Amin alijitaja kuwa *"Conqueror of the British Empire"* na aliendesha utawala wake kwa hofu na udikteta.

Inakadiriwa kuwa watu kati ya 100,000 hadi 500,000 waliuawa wakati wa utawala wake, huku kundi kubwa likiwa wapinzani wa kisiasa, wanajeshi wa zamani, viongozi wa kidini, na makundi ya wachache, kama Wahindi na Waafrika wa Asia. Mnamo 1972, Amin alifukuza Wahindi wapatao 60,000 kutoka Uganda, hatua iliyoathiri uchumi wa taifa hilo kwa kiasi kikubwa.

**Anguko na Kimbilio**

Mwaka 1978, utawala wa Amin ulianza kudhoofika baada ya kuanzisha vita na nchi jirani ya Tanzania. Jeshi la Tanzania likishirikiana na wapinzani wa Uganda, walifanikiwa kumuondoa madarakani mwaka 1979 baada ya vita iliyomalizika kwa kutwaliwa kwa jiji la Kampala. Amin alikimbilia uhamishoni, awali Libya, kisha akahamia Saudi Arabia ambako aliishi hadi kifo chake mnamo Agosti 16, 2003.

**Urithi na Tathmini**

Idi Amin anakumbukwa kwa utawala wake wa kikatili, ukiukwaji wa haki za binadamu, na kuharibu uchumi wa Uganda. Ingawa kuna baadhi ya wananchi waliomkumbuka kwa kuboresha miundombinu ya kijeshi na kuhimiza uzalendo kwa njia zake za udhalimu, wengi wanamtazama kama mmoja wa madikteta wabaya zaidi katika historia ya Afrika.

Huyu ni Idd Amin Dada, *Conqueror of the British Empire*

*RM*

# SAKO KWA BAKO:

## WASEMAVYO WASOMAJI...

"Maoni yangu kwa watanzania wote waishio ndani na ya nchi tuipende lugha yetu ya kiswahili, Tupende kusoma vitabu na makala za kiswahili.
Tuwaunge mkono waandishi wetu wa Hadithi na vitabu mbalimbali wanaotumia lugha ya Kiswahili kwa kununua na kusoma kazi zao."

**Mwl. Patrick Nkika**



"Natamani watu watambue siri iliyojificha kwenye vitabu na kuamua kuitafuta. Pia, nawashauri wazazi kuwanunulia watoto vitabu ili wasome. Tabia ya kusoma ikianza kujengeka tangu utotoni, inakomaa vizuri na mwisho wake ni kuwa na taifa bora hapo baadaye.

**Rebeca Kitomari**



"Wito wangu kwa wazazi wa kitanzania naomba tuwajengee watoto utamaduni wa kujisomea vitabu na kupunguza matumizi ya simu na michezo isiyokuwa na ulazima kwani itawajengea tabia ya udadisi pamoja na kuwapa maarifa mapya ambayo yatawasaidia katika maisha yao."

**Martin Mazungwa**



"Wandishi wa vitabu nawambia zipendeni kazi zenu na msiogope wa somaji pale wanapo taka kujua visa vya vitabu vyenu. Wengi wenu hampendi kuulizwa maswali tena mnachukia. Mimi mmojawapo, napenda kuwauliza maswali waandishi, lakini wengi wananichukia kwa kuwaulizauliza"

**Zamira Sanguti**




Ngurumo ya Mwandishi tunakushukuruni nyote mliyotoa michango yenu mbalimbali kati safu za jarida hili. Ujumbe wenu umefika sawia kwa wote wanaosoma jarida hili. Naamini kwamba kupitia maneno yenu wapo waliobadili tabia na kujikuta kuwa sasa ni wasomaji wazuri sana.

Shabaha yetu kubwa ni kuwafanya watu wawe na uraibu huu wa kusoma, iwe vitabu, magazeti na hata vipeperushi, yaani mtu ajisikie kusoma kusoma kusoma… hakika kusoma ni kuzaliwa upya.

# SHAJARA YA MUUAJI—7

Na. Richard Mwambe



***Aziza, ulikosa nini mpaka unatembea na kijana huyu mchafu asiyejua sabuni? Ona sasa uzuri wako wote umeishia mochwari!* Akaendelea kunung'unika kana kwamba marehemu alikuwa mkewe au bibi yake.**

**Endelea...**
Damasi bado alikuwa hajaamini kama Magena alikuwa mpenzi wa siri wa Aziza maana walikuwa watu wa madaraja tofauti.
Ndani ya *lockup,* Magena alipokewa na vijana wengine pamoja na Mathias Marengo. Mathias na Magena hawakujuana kabisa kama wote wanakabiliwa na kesi moja. Magena alilia kumuomboleza Aziza. Aliikumbuka siku ambayo alikutana na mwanamke huyo mpaka akampa jina Malkia wa Nguvu.

❦ ❦ ❦

**2010, April 3**
Ilikuwa usiku wa saa saba, Magena akiwa kajilaza kwenye kilago chake ndani ya chumba kidogo alichopanga kwa Mzee Mtengela. Mtengela, mzee wa kizaramu aliyejenga katika Mtaa wa Maguruwe miaka na miaka ndiye pekee aliyegoma kuuza eneo hilo kwa matajiri. Alimpokea Magena miaka minne iliyopita akiwa kaja mjini kutafuta maisha. Chumba cha uani kwa kodi ya shilingi elfu tano kilimfaa. Magena akiwa katikati ya usingizi miaka miwili kabla ya tukio hili, alishtushwa na hodi iliyobishwa kwa fujo. Akakurupuka na kuuliza "nani, mbona usiku!"
"Samahani nifungulie kaka angu!" Ilikuwa sauti ya kike. Mwanamke aliyekuwa akihema kama anakimbizwa. Magena akafungua mlango ule wa madebe yaliyojaa kutu. Macho yake yakakutana na taswira ya mwanamke. Kabla hata hajauliza, yule mwanamke akaingia ndani na kumtaka Magena kufunga mlango.
"We ni nani?" Magena akauliza.
"Yule mwanamke alikuwa akitweta huku mkono wake wa kuume uliopendezeshwa na Pete aghali ukiwa umeshika kifua chake.

Mwanga hafifu uliotokana na taa ya chemli iliyokuwa ikiwaka ndani ya kijichumba hicho iliongeza uzuri wa mwanamke huyo.
"Usinishangae, mi siyo jini..." yule mwanamke akamwambia Magena huku akionesha miguu yake Ili Kumdhihirishia kwamba yeye siyo jini. Si wanasema kuwa jini ana kwato za ng'ombe! Mi sijui.
"Usiku huu unafanya nini...nje?" Magena akauliza.
"We acha tu, siwezi kukudanganya, nimefumaniwa hapo gesti ya mtaa wa tatu. Nilipokimbia nikaona hapa kimlango kiko wazi nikaingia kujificha! Nisaidie nilale nitaondoka alfajiri," yule mwanamke akaeleza. Magena akatikisa kichwa. "Utalala wapi sasa? Mwanamke mzuri, mrembo, tajiri kama wewe, utalala hapo ninapolala Mimi?" Akamuuliza.
"Hapahapa nitalala..." Akajibu yule mwanamke na kutoa kanga kwenye pochi lake, akatandika juu ya kile kilago na kujilaza. Mh! Ilikuwa Shida kwa Magena baada ya macho yake kuona mnyumbuliko wa mwili wa kike pale chini. Akajikuta akikabiliwa na mgogoro wa nafsi. Bukta aliyovaa ikaanza kumbana. Akabaki palepale juu ya dumu la maji alilokalia, machoye yakisadifu ufundi wa hali ya juu wa Baba Muumba.

"Njoo ulale!" Sauti ya yule mwanamke ikamwambia Magena. Ilikuwa ngumu kwake kukubaliana na alichokisikia. Mwito ule ukarudiwa mara tatu. Magena akajilaza kando ya yule mwanamke. Yaani, Aziza. Kimvua chepesi kilichokuwa kikipiga huko nje kiliwafanya wawili hawa kugusanagusana miili yao. Magena hakupata usingizi maana mwili wake ulipata tabu. Mara alale hivi mara vile. Na alipojikuta amezidiwa akageuka upande wa Aziza. *Liwalo na liwe!* Akajisemea.

Si kwamba mwanamke huyo alikuwa mvumilivu, hata yeye alipata shida. Kisa cha kujilaza kugeukia ukutani ni kwa sababu macho yake yaliweza kuona upenyo wa bukta ya Magena kila alipojisahau na alichokiona kilimpa wakati mgumu. '*Njoo tulale*' ndilo aliloona labda litakuwa chambo. Akiwa kampa mgongo Magena, Aziza alihisi kuguswa na kitu cha motomoto, kilichomfanya ashushe pumzi ndefu. Harufu ya Magena ilimsumbua kidogo na uzito wa hewa mule ndani ulikuwa mkubwa, afanyeje. Lisaa limoja lililofuata, tayari mmoja alikuwa juu ya mwenzie, shughuli nishughulikie.

Usingizi ulipowapitia, walishtushwa na swala al-fajir iloyoimbwa kutoka msikiti wa nyuma tu. Na wakati huo Mzee Mtengela alikuwa tayari keshaamka.
"Kumekucha naomba niende!" Aziza akamwambia Magena.
"Subiri Mzee aende msikitini..." Akamjibu. Aziza akatulia kusubiri.

# SHAJARA YA MUUAJI—7

Katika subira hiyo, nusu saa ilitosha kushughulikiana tena. Aziza alikuwa hoi kwelikweli. Nafsini mwake alikiri hajawahi kutana na shughuli nzito kama hiyo. Akaondoka na kusindikizwa na Magena.

"Nitakutafuta! Nikushukuru kwa yote!" Aziza akamwambia Magena huku akichukua namba yake. Tangu siku hiyo, Aziza aliposikia ashki zinazohitaji shughuli nzito humpigia Magena, na Magena alijua vyema anachopaswa kutenda. Alimshughukikia. Hata yeye hakuamini, aliona kweli wimbo wa Profesa J, *Zali LA Mentali,* una maana kubwa.
Aziza alikuwa kahaba, aliyeuza mwili wake kwa watu tofauti tofauti. Alipopata mwanaume ambaye hakuweza kumfikisha sawasawa basi alimwita Magena amalizie kazi. Hata siku mauti yalipomkuta ilikuwa hivyohivyo.
Nani kamuua Aziza, Magena Makange au Mathias Marengo?

**2015, March 27**
INSPEKTA Msaidizi wa Polisi, Ngai Mathola aliwasili katika kituo cha polisi Chang'ombe. Hiki kilikuwa kituo chake kipya cha kazi alichopangiwa baada ya kuhamishwa kutoka Dodoma. WP Nghai Mathola alijulikana sana kwa uchapa kazi wake. Huko alikotoka, alipambana na kuwanyoosha wavunja sheria wengi sana. Aliyesuluhisha migogoro migumu iliyoshindikana.
Katika kituo kikuu cha polisi cha Dodoma, ndipo Mkaguzi msaidizi wa polisi, Ngai Mathola alipohudumu. Sifa zake za kutenda lililo haki kwa wananchi ndizo zilizomfanya aishi na watu. Waswahili wanasema *'kaa na watu uvae viatu'*. Ngai alivaa viatu. Alikuwa askari polisi wa kike yaani WP. Mrefu kiasi mwenye mwili wa wastani. Kwa urefu wake, hatuwezi kusema kuwa ni mnene au mwembamba, itoshe tu kusema kuwa alikuwa na mwili mkakamavu na akili yenye kuamua vizuri. Ngai Mathola alikuwa mpelelezi kwa asili. Kama kuna kazi aliyoipenda basi ni upelelezi, kutengua vitendawili vilivyoshindikana.

**Tsh 4000/= Softcopy. Lipia Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Whatsapp 0766974865**

Akiwa Dodoma ndicho kitengo walichompatia, alifanya kazi chini ya afisa upelelezi wa mkoa. Alifanya vizuri mpaka hata sifa zake zikampita bosi wake.

"Karibu sana," sauti nzito ya kiume ikamkaribisha. Ngai alisimama kwa ukakamavu mbele ya mkuu wake mpya, OCS S.P Steven Sabasi.
"Asante afande!" Ngai akajibu kwa sauti iliyotimia.
"Hapa ni Chang'ombe..." S.P Steven huku akiwa amesimama akamwambia Ngai, "...Dodoma yote ile, ni sawa na nusu wilaya ya Temeke, siyo kwa ukubwa wa eneo, bali kwa kipimo cha uhalifu ... Jisikie upo nyumbani. Hapa ni tofauti, ofisi uliyokuwa nayo Dodoma, siyo utayoihudumia hapa... Namaanisha hapa hautakuwa mpelelezi," akamwambia.

Ngai akabaki kimya akisikiliza kila agizo. Katika jeshi la polisi, kila asemalo mkubwa wako, jibu ni *'ndiyo afande'*.
"Ndiyo afande!" Akajibu pasi na kupepesa macho.
"Tuliomba tupatiwe mtu wa rekodi... Tumeletewa wewe, hivyo ofisi yako itakuwa ni *recording*... Najua unaelewa kwa kuwa umeisomea..." SP Steven akamaliza. Akamtazama WP Ngai kutoka juu hadi chini, ametimia. Kofia safi nyeusi yenye *crown* iliyong'aa udhahabu wake. Suti yake ya kipolisi ya khaki, nyota yake iliyong'aa begani, fimbo iliyobanwa kwapani na kiatu safi viliudhihirisha uafisa wake. WP Ngai Mathola alikuwa nadhifu, mkakamavu na mwenye nidhamu ya hali ya juu. Steven akainua simu ya mezani na kubonya tarakimu fulanifulani. Sekunde tu upande wa pili ukapokea. Akaongea maneno machache na kuitua.

***Itaendelea toleo lijalo...***

**Wakavuta hatua na kuingia katika hoteli ile. Hakuna aliyewauliza lolote kwa kuwa vijana wa Mathis hawakuwa wageni machoni pa raia wa Nigeria hasa katika mji huo. Wakapanda ngazi kama kwao na kuufikia mlango walioelekezwa.**

---


***Endelea***

Pigo moja la nguvu mlango ule ukaachia na kubaki wazi. Vijana wale wanne wakasimama ndani ya kile chumba kisha akaingia kijana wa tano aliyevalia suti safi na kusimama mbele ya wote, akaondoa miwani yake myeusi usoni na kuipachika katika moja ya mifuko ya koti lake. Codec alikuwa palepale alipoketi akitazama yote hayo. Hakuonesha kuogopa wala kutetereka kwani alishayazoea kutokana na kazi yake.

Yule kijana wa tano akamwendea Mirabel pale kitandani, akamkuta bado akilia kwa vikwifukwifu, akamnasa makofi matatu na mirabel akaanza upya kulia kwa uchungu.
Aliponyoosha mkono wake, akakabidhiwa *'Mkia wa Taa'* na kumtandika mwanamke yule viboko vya kutosha mpaka akapoteza fahamu. Alama za kiboko kile zilibaki kama muhuri wa uchungu juu ya mgongo laini wa binti huyo.
"Unalijua kosa lako, na Mathis anahitaji akuone," akasema kisha akamtazama Codec, "unajiita Ric Sewer, umepatikana Codec, kama wewe ni Code C basi sasa utakutana na Code A," aliposema hayo akawatazama vijana wake, "waleteni huku!" akawaambia kisha yeye akatangulia kutoka nje.
Ghafla Codec akajikuta mbele ya mitutu miwili ya bastola, hana ujanja.
"Simama taratibu tuondoke, ukijifanya mjanja tunakumaliza," kijana mwenye bastola akamwambia huku akimpa ishara Mzungu huyo atoke nje. Codec akatoka taratibu pale alipokuwa ameketi lakini kabla hajamaliza ile meza, akainua ile bilauri iliyojaa pombe na kummwagia usoni yule aliyemwamuru.
Wakati huyu akikwepa kinywaji kile ile bilauri ikaishia katika kichwa cha yule wa pili mwenye bastola. Codec akavuta hatua moja kubwa na kumfikia yule wa kwanza. Konde moja zito likatua shavuni na kuvunja meno kadhaa. Akaudaka mkono wenye bastola na kugeuka naye kisha akafyatua risasi zilizowalaza wawili chini bila uhai.

"Hellllpppp!" aliyebaki akapiga kelele za msaada. Wakati huo Codec tayari keshatoka dirishani na kujibwaga juu ya nyumba ya pembeni, akarukia nyingine na kutua katika pipa kubwa la takataka nazo zikamfunika juu yake. Akatulia kimya. Jamaa wakasaka na kusaka huku na kule wasi mwone, walipochoka wakaamua kuondoka zao kurudi kwa bosi.
Huku nyuma Codec akaibuka kutoka kwenye zile takataka, akatoka taratibu na kutua nje. Bado giza nene lilikuwa limetawala ule mji, alipoitazama saa yake, ilikuwa imetimu saa tisa inaelekea saa kumi. Muda unanikimbia, akawaza na kutembea haraka haraka mpaka kwenye ile hoteli akaingia bila kuongea na mtu. Alipofika chumbani kwake akakuta zile maiti bado zipo vilevile, damu imetapakaa huku na huko, akamtikisa Mirabel. Katulia tu. Akambeba na kumpeleka bafuni akamfungua bomba la maji baridi, msichana huyo akashtuka na kuanza kuhema kwa nguvu.

"Amka mtoto mzuri amka!" akajikuta akimwamsha kwa nguvu na




Mirabel akarudi katika hali yake lakini alikuwa akilalamika maumivu. Akamsaidia kumtoa katika maji maana alijua hapo hapafai tena kuishi. Akamsaidia kuvaa harakaharaka kwani pale kitandani alikuwa nusu utupu. Dakika kumi baadaye walikuwa nje ya hoteli hiyo kwa kupitia mlango wa nyuma. Codec akachukua taksi na kuondoka eneo hilo.

❦

Saa kumi alfajiri walifika kwenye lodge inayojulikana wa jina la Chief Okuodor iliyokuwa nje kidogo ya mji. Hapo Codec akapata chumba pamoja na Mirabel, walipojifungia tayari na kuhakikisha usalama wa kila kitu, Mirabel akajitupa kitandani.
"Kumbe jina lako sio Ric!" akamwambia.
"Ndiyo, naitwa Codec au Code C," akajitambulisha.
"Kwa nini ulinificha?"
"Hiyo ni moja ya kanuni za usalama wa maisha yako, hata wewe kwa mtu usiyemjua hutakiwi kumpa

jina lako kamili mara moja…"

"Ok! Mtalii gani anajua kuua namna ile?" akamkatisha kwa swali.

"We umeonaje nimeua wakati ulizimia? Kwanza langu bado hujalijibu. Wale jamaa wamekulaumu kuwa ulikiuka moja ya kazi, haya niambie ni kazi gani? Mimi ni muuaji *by professional,* hivyo usiponipa jibu sahihi nakuua bila shaka na huna thamani kwangu," Codec aliongea huku akiichomoa bastola yake na kuiweka sawa.

"Hadithi ndefu sana, usifikiri nafanya kazi kwa Didiof kwa kutaka, bali ni kwa shuruti…"

"Kivipi?"

"Didiof alikuja kijijini kwetu miaka nane iliyopita kwa minajiri ya kununua ardhi. Tayari mkononi mwake alikuwa na kibali kutoka serikalini na eneo alilolitaka lilikuwa ni shamba la baba yangu ambalo ndani yake ndipo kulikuwa na nyumba tunayoishi. Baba yangu alikuwa jeuri na sheria aliijua, akamshitaki Didiof na huyo aliyemuuzia eneo hilo. Kesi ile ilikuwa kubwa sana na Didiof alijitahidi kuhonga pesa huku na kule lakini bado mzee wangu hakukubali, yeye alikuwa akiwazidi kwa vifungu vya sheria.

Siku moja alikuja nyumbani asubuhi na kumwomba baba akafunge ile kesi. Akamwahidi kumlipa pesa nyingi ambazo zingemjengea nyumba nyingine na kubadili hali ya maisha ya familia yetu. Baba bado alikataa katakata, na akasema wazi kuwa hatoweza kufanya kitu kama hicho. Ndipo Didiof alipomwambia baba 'Nitakuonesha kuwa sisi ndiyo wenye nchi, kiwanja nitachukua na hutofanya lolote maana utakuwa mfu'. Baba yangu akaenda kushitaki kwa kuwa katishiwa maisha. Siku aliyotakiwa kufika mahakamani kwa kesi hiyo kusikilizwa… Usiku uliotangulia, wafuasi wa Didiof wakafika nyumbani na kuteketeza familia yote, walimuua baba, mama na kaka yangu, walipotaka kuniua mimi kiongozi wao akawazuia wakanichukua mpaka mjini kwa Didiof. Wakamweleza kuwa hawakuniua kwa sababu waliona nafaa kuwasaidia katika maeneo fulani ya kazi zao.

Basi, kipindi hicho nilikuwa msichana wa miaka kama kumi na mbili hivi, nikakaa kwa tajiri huyo lakini kilichoniuma tena ni kutumikishwa kingono na mtu huyo asiye na aibu…" Mirabel akaanza kulia kwa uchungu. Codec akaingiwa na huruma, akaitua bastola yake na kumkumbatia msichana huyo.

"Pole sana, pole sana Mirabel…"

"Hapana siitwi Mirabel, naitwa Odette!" alitaja jina lake halisi kwa mwanaume huyo mtu mzima. Hakika hakuna mkweli duniani, ukweli uko moyoni mwako tu! Codec akawaza na kisha akamtazama binti huyo na kuzikutanisha sura zao.

"Odette, kwanza kabisa lazima ujue kuwa baba yako anakutazama kwa lile unalofanya, damu yake ilimwagika katika kutetea ardhi ya kaya yake isipotee. Huna budi kulipiza kisasi kwa mtu huyo. Didiof ni mnyama, unyama aliyokufanyia wewe na familia yako ameufanya mahali pengi duniani hata mimi niko hapa kumsaka yeye na sintompa nafasi ya kupumua," Codec aliongea kwa hasira na kumpandikizia chuki msichana huyo.

"Lipa kisasi, baba yako na mama yako watafurahi na kukupa baraka zao huko waliko. Huyu ni mwanadamu au mnyama kwako? Kakuulia baba, mama na kaka, kachukua ardhi yenu na kakuchukua wewe tena akakutumikisha kingono bila ridhaa yako, kakubaka. Una uamuzi mmoja tu moyoni mwako," akaichukua ile bastola na kuigeuza kitako kumwelekea mwanamke huyo.

"Shika, *kill him now!* Najua wewe unaweza kumfikia kiurahisi…"

"*No!* siwezi na sijawahi kuua mtu…"

"Mirabel, hujui kuwa ukimwua Didiof utakuwa umewalipizia kisasi watu wengi sana? Huoni kuwa utakuwa umeokoa mateso mengi ambayo mwanadamu angeyapata kuanzia jua la leo litakapochomoza? Kama mtu mmoja analeta taabu kwa maelfu ya watu kwa nini aishi? Ni lazima afe. Afe kwa ajili ya wengi. Shika hii, kuua mtu ni rahisi sana, unaweka kidole hapa unavuta nyuma basi! Risasi moja kwenye paji la uso, au ya moyoni umemaliza kazi…"Maneno hayo ya Codec yalimwingia barabara Mirabel. Akakumbuka wengi ambao kweli wamepata mateso kutokana na mtu huyo. Kuna waliotekwa, waliobakwa, waliofanyiwa majaribio ya madawa ya kulevya na afya zao kuharibika, walionyang'anywa mashamba na wengine kuuawa kama ilivyokuwa familia yake. Moyo wa Mirabel ukajikusanya na kuanza kulowa kwa hasira na uchungu.

"Ni ngumu… wataniua mimi kwa kuwa sina uzoefu wa kazi hii…"

"Nikusaidie?" C odec akauliza.

***Itaendelea toleo lijalo***

# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (13)

**“Hii alama haikuwa hapa kabla” Marjane alijisemea moyoni. “Mara ya kwanza alama nyeupe, na mara hii tena alama nyekundu!! Vizuri sana! Nitafanya kama nilivyofanya mara ya kwanza.”**

**Endelea...**

Aliingia ndani na kwenda kuchukua chaki nyekundu. Kisha akarudi nje na kuweka alama nyekundu katika kila fremu ya dirisha kwenye nyumba zote za mtaa ule.

“Hii lazima imchanganye huyu aliyeweka ile alama nyekundu pale.” Alijisemea huku akicheka. Kisha akarudi nyumbani kuendelea kuandaa chakula cha jioni, lakini hakumwambia yeyote kuhusu alama ile nyekundu.

Yule mwizi aliyeweka ile alama nyekundu alifika msituni, alipowakaribia wezi wenzake akaanza kupiga kelele za furaha, “Nimeiona! Nimeipata nyumba ambayo suti ya marehemu ilishonwa!!”

Kiongozi wao alimfurahia sana. “Umefanya kazi nzuri!” Alisema. “Umefanya kazi muhimu sana! Sasa tunaweza kumpata aliyetuibia dhahabu zetu.”

“Nilienda mpaka kwa fundi nguo, Mustafa.” Mwizi alisema kwa kujisifu. “Alikubali kunisaidia kama ningempa dhahabu. Nikamfunga macho na kitambaa kama alivyofanya awali, na akanipeleka mpaka kwenye hiyo nyumba. Nikaweka alama ndogo sana nyekundu kwenye fremu ya dirisha ili tuweze kuipata hiyo nyumba tena.”

Wezi wakampigapiga mgongoni kama ishara ya kumpongeza huku wakishangilia. Kisha kiongozi wao akasema, “Nipeleke huko sasa hivi.”

Hivyo basi, wawili hao wakaondoka kuelekea mjini. Baada ya kufika tu mwizi mmoja akamuonesha mkuu wake nyumba ambayo kwenye dirisha kuna alama nyekundu kwenye fremu.

“Hii hapa sasa!” mwizi alimwambia mkuu wake. “hii ndiyo nyumba yenyewe! Unaona alama nyekundu kwenye fremu ya dirisha?”

Kiongozi wa wezi aliendа mpaka karibu na kuiangalia alama ile.

“Ndiyo, naiona! alijibu mkuu wa wezi. “pia naona kuna alama kama hii katika fremu ya dirisha katika nyumba ile, na ile pia! Na ile na ile! Kwanini alama hiyo ipo kila dirisha katika nyumba za mtaa huu? Nani atakuwa ameziweka hizo?”

“sijui, “ alisema mwizi yule akiwa hana furaha tena. “Mimi niliweka alama kwenye dirisha moja tu”

“wewe ni mjinga wa pili!!” alifoka mkuu wao. “haya haraka sana turudi msituni!!”

Asubuhi iliyofuata, kiongozi wao aliwaita wezi wote katika eneo lao la kukutana.

“Wawili wenu walishindwa kuitafuta nyumba tunayoihitaji” aliwaambia. “Sasa nitakwenda na kuitafuta nyumba mimi mwenyewe. Nisubirini hapa”

Hivyo basi, kiongozi wao akaondoka kuelekea mjini mwenyewe. Akaonana na Mustafa katika kibanda chake, akampa sarafu ya dhahabu. Mustafa akamuongoza kiongozi huyo wa wezi kulekea kwenye ile nyumbaya Kassim.

Kama kawaida alivaa kitambaa kufunika macho, na kwa kutumia msaada wa harufu na sauti mbalimbali, Mustafa alifanikiwa kumfikisha kiongozi wa wale wezi mpaka kwenye ile nyumba.

“Nasikia harufu ya maua mazuri sana, natumaini hapa ndipo mahala penyewe.” Alisema Mustafa.

“Sitaweka alama yoyote ya chaki,” kiongozi yule alijisemea moyoni. “Alama za chaki zote zilizowekwa hazikuweza kufaa kabisa hapo kabla. Nitaitizama nyumba hii kwa umakini kabisa na kukariri kila kitu ili niweze kukumbuka ninachokiona.

Hivyo basi, Kiongozi yule aliangalia madirisha mazuri ya nyumba ile, pia aliangalia milango iliyopakwa rangi ya samawati na mapazia mekundu yaliyoning’inizwa kwenye madirisha. Aliangalia mimea mirefu iliyopandwa ndani ya mitungi mikubwa meupe na paka wa rangi ya machungwa mwenye macho ya njano akiwa kwenye dirisha akimtazama.

Baada ya kuangalia yote hayo, alimchukua mzee Mustafa na kumrudisha kwenye kibanda chake kisha akarudi msituni kuonana na watu wake.

mpango wa kiongozi wao.

***Itaendelea toleo lijalo***

ILIKUWA nderemo na vifijo katika ukumbi wa mikutano wa Julius Nyerere (JNCC) jijini Dar es salaam wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan alipozindua kitabu kipya cha maisha ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Edward Moringe Sokoine.

Hafla hiyo iliyofanyika siku ya tarehe 30 Septemba, ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, waliopo sasa na waliopita, ndugu na jamaa wa familia ya Sokoine. Pamoja nao walikuwapo wadau wa masuala ya vitabu pamoja na wawakilishi wa mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Hiki ni kitabu cha pili kinachohusu maisha ya Hayati Edward Moringe Sokoine. Kitabu hiki chenye anwani 'EDWARD MORINGE SOKOINE MAISHA NA UONGOZI WAKE' kimeandaliwa na Taasisi ya Uongozi Chuo Kikuu cha Sokoine.

Kama hayo hayatoshi, akiieleza jamii ya Kimasai na Kiafika ya wakati huo ilivyomuweka chini mwanamke, Sokoine ndiye aliyeruhusu wanawake kuandikishwa jeshini.

Pia alimshukuru makamu wa Rais kwa kuhimiza na kuhakikisha kitabu hicho kinakamilika na yeye kuwa mwandishi wa dibaji. Kwa kupitia jukwaa hilohilo alimsisitiza Rais wa awamu ya nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kumaliza kitabu chake mapema ili kizinduliwe hapo.

Katika hafla hiyo masimulizi mbalimbali ya maisha ya Hayati Edward Moringe Sokoine yalisimuliwa. Burudani kutoka vikundi mbalimbali viliifanya siku hiyo kuwa njema na ya kuvutia.

Kitabu hiki, sasa kipo madukani kwa bei rafiki na kimeandikwa kwa lugha aushi ya Kiswahili.


## RAIS WA J.M.T DR. SAMIA SULUHU HASSAN AZINDUA KITABU KIPYA CHA SOKOINE

Hayati Edward Moringe Sokoine alizaliwa tarehe 1 Agosti, 1938. Yeye ni kutoka Monduli katika jamii ya Wamasai. Aliwahi kuwa Waziri Mkuu mara mbili; kuanzia tarehe 13 Februari 1977 hadi 7 Novemba 1980 na 24 Februari, 1983 hadi kifo chake 12 April, 1984.


Edward Moringe Sokoine alifariki kwa ajali ya gari tarehe 12 April, 1984 katika eneo la Dakawa, Morogoro akiwa safarini kutokea Dodoma kuelekea Dar es salaam. Kifo chake kilileta majonzi makubwa kwa Watanzania wa kawaida ambao walikuwa wanamtarajia kuwatetea wanyonge na kuinua hali ya maisha yao.

Mwili wake ulizikwa nyumbani kwao Monduli, mkoani Arusha.

Katika hotuba yake ya uzinduzi, Rais Dkt. Samia alimtaja Sokoine kama kiongozi aliyeheshimu mamlaka za uteuzi wake na kumsifu kwa sifa zake za uaminifu nidhamu na uchapakazi. Pia alimtaja kama kiongozi aliyekuwa na maadili mema kiasi kwamba alipata vyeo vingi serikalini akiwa na umri mdogo.



**Inasemekana kuwa hii ndiyo riwaya fupi kuliko zote… sasa kama ni hivyo kwanini haijaingia kwenye kitabu cha rekodi za dunia?**



Ernest Hemingway

**"For sale: baby shoes, never worn."** Hii inasemekana ndiyo riwaya fupi zaidi ulimwenguni. Riwaya hii imeandikwa na Ernest Hemingway, wengi tunmjua umahiri wake katika fasihi.

Hii inahesabiwa kuwa riwaya fupi zaidi kutokana na uwezo wake wa kueleza hadithi kamili kwa maneno sita tu.

Riwaya hiyo fupi inayoaminika kuandikwa na Ernest Hemingway inajulikana kama mfano maarufu wa "hadithi fupi sana" au "flash fiction." Hadithi hiyo ina maneno sita tu: **"For sale: baby shoes, never worn."** Ingawa hadithi hii ni fupi, inasababisha athari kubwa kihisia kutokana na athari ya ubaguzi na tafsiri zinazoweza kufanywa.

Kwa muda mrefu, imekuwa maarufu kwa sababu ya uwezo wake wa kuibua maoni mengi juu ya kinachotokea nyuma ya maneno hayo machache. Watu wengi huona kuwa kuna hadithi ya huzuni, ikimaanisha kwamba kuna sababu mbaya ya viatu vya mtoto kuuzwa bila kuvaliwa, labda kutokana na kifo cha mtoto huyo au hali nyingine ya huzuni.


Hata hivyo, kuna ushahidi mdogo wa kihistoria unaothibitisha kuwa Hemingway aliandika hadithi hii, ingawa imekuwa sehemu ya simulizi ya maisha yake ya uandishi. Hadithi hii hutumika mara kwa mara kuonesha nguvu ya uandishi wa hadithi fupi na jinsi maneno machache yanaweza kuelezea hadithi kubwa yenye hisia na maana.

Ni mfano wa kipekee unaoonyesha uwezo wa lugha kuwasilisha hadithi kamili kwa njia ya ufupi sana, na ndiyo sababu imekuwa maarufu ulimwenguni kote.
Hadithi hii fupi **"For sale: baby shoes, never worn"** haijaingia rasmi kwenye Kitabu cha Rekodi za Guinness kama riwaya fupi zaidi. Ingawa inajulikana sana na inaheshimika kama mfano wa uandishi wa hadithi fupi, haijaandikwa kama rekodi rasmi katika kitabu hicho.

*Guinness World Records* kwa kawaida hutambua rekodi zinazoweza kuthibitishwa na kupimika moja kwa moja. Kwa kuwa hadithi hii inahusiana zaidi na fasihi na tafsiri za kisanii, inaweza isiwe na vigezo vya moja kwa moja vinavyohitajika kuingia kwenye rekodi za Guinness.

Hata hivyo, hadithi hii inabaki kuwa maarufu kwa watu wengi ulimwenguni kutokana na uwezo wake wa kuwasilisha simulizi kamili kwa maneno machache. ***N.M***

# THINK LIKE A CHAMPION by. Donald J. Trump



**Kitabu: Think Like a Champion**
**Maktaba; ANNA MBISE MOBILE LIBRARY**
**Msomaji; FERNADI YARRO**
**Mkoa: Dodoma**

**1 . WEKA PICHA KUBWA AKILINI KWAKO**
Mwandishi anatueleza kuwa unapotaka kufanya jambo kubwa inabidi uweke picha ya kile unachotaka kukifanya mfano kama ni biashara, kampuni, kilimo n.k. Weka picha kubwa ya hayo mambo ili ujue unatakiwa uchukue hatua zipi, kuifanya picha hiyo kuwa vitendo halisi. Hii itakupa hamasa ya kufanikisha jambo lako.

**2. UTHUBUTU.**
Tuwe na uthubutu na dhamira ya dhati ya kutekeleza jambo letu bila kuwa na wasiwasi au uwoga kwani uoga hauna faida yoyote bali utatufanya tushindwe kufikia malengo yetu. Bwana Trump anatuasa tusiogope kufanya jambo kubwa kwa ajili yetu na jamii yetu, kwani hakuna mwingine mwenye kukufanyia zaidi yako wewe.

**3. ZUNGUKWA NA WATU MUHIMU ZAIDI**
Hawa ni watu watakao kushauri, kukufundisha, na kukushika mkono pale unapowahitaji kufanikisha jambo lako. Pia wawe ni wale waliokuzidi katika sekta unayotaka kuwekeza. Zungukwa na watu bora Zaidi katika kada unayotaka kuifanyia kazi, wasomi, wajasiriamali n.k Ndio tuangalie watu wakushirikiana nao. (*naongezea ya kwangu Kuwa karibu na uwaridi unukie)*

**4. FIKIRIA KAMA(Genious)**
Tuwe na mawazo sahihi na makubwa ambayo yatafanya mambo madogo kuwa makubwa, kwani mambo makubwa yanafanywa na fikra kubwa, huwezi kufikiri padogo ukafanya makubwa, (kuna msemo wa utavuna ulichokipanda ) Ukipanda mawazo makubwa utavuna makubwa ikipanda madogo utavuna kidogo, hivyo tufikiri kikubwa zaidi.

**5. UBUNIFU**
Mwandishi anatukumbusha tuwe wabunifu wa mambo mapya na namna tutakavyoweza kuwa tofauti na wenzetu katika kutekeleza mambo. Hii itajenga kuaminiwa na watu wengi pale ubunifu wetu utakapo kuwa na mchango na faida kwa jamii. Tutapata thamani ya juu mbele ya jamii hivyo na huduma zetu zitakuwa kwa viwango vikubwa.

**6. KUJIFUNZA ZAIDI;**
Tunakumbushwa kujifunza zaidi na zaidi kwa mambo ambayo hatuyafahamu. Njia pekee ya kuyafahamu mambo ni kujifunza mfano. Kusoma vitabu mbalimbali mwandishi anapendekeza tusome vitabu kama (The Art of War by Tzu) ili tujifunze mbinu mpya ya kujenga mafanikio yetu katika nyanja mbalimbali.

**7. MAWAZO CHANYA**
Mwandishi anatueleza faida ya kuwa na mawazo mazuri ambayo yatatufanya tufanikiwe maishani. Tutakuwa na amani, furaha na msukumo mzuri katika kukabiliana na Changamoto zinazojitokeza katika maisha, tunapaswa tuwe na mawazo ya kujenga zaidi, ya ushindi, mafanikio, kuliko fikra za kushindwa, fikra za kusononeka, fikra hasi zote hazitakiwi tunapofanya jambo lolote.

**8. FANYA KWA UHARAKA, UFUPI**
Mwandishi anatueleza njia ya kuwa na mafanikio ni kufanya kwa uharaka na kwa ufupi zaidi. Hapa tutaokoa muda wakutekeleza mambo bila kuchukua muda mrefu na kutumia nguvu nyingi sana, tuepuke kutumia muda mwingi kwa jambo moja tuokoe muda, maana hata mitihani ya darasani ina muda maalum usipomaliza ndani ya muda mfupi ni sawa na kushindwa, hivyo tunapaswa kutumia muda vizuri tunapo fanya mambo yetu na ili tuone mafanikio ya haraka.

**9. MAKOSA NA CHANGAMOTO.**
mwandishi anatuasa tujifunze kutokana na changamoto na makosa tunayoyafanya, ili uwe bora zaidi unapswa kujifunza kwenye makosa na pale tunapojisahihisha tutakuwa imara na watu bora katika maisha. Tusione tu changamoto na kuishia kulaumu na kusononeka tujifunze namna ya kutokurudia changamoto za namna hio. (Wahenga wanasema kisichokuua kitakupa fundisho).

**10.WAAMBIE WATU MAFANIKIO YAKO.**
Mwandishi anatuasa tukifanikiwa katika maisha yetu tusiache kuwaambia wengine, ili iwe hamasa kwao. Hapa utawahamasisha watu wengi kutaka kufanikiwa kama wewe na pia itakuwa furaha na amani kwako binafsi unapowaona watu wakifanikiwa kupitia wewe. Pia itajenga jamii iliyo bora na yenye mafanikio. Hapa napata mfano wa dada @MbiseAnna kwani kupitia yeye na maktaba yake leo sisi wasomaji tunapata maarifa mengi yanayotusaidia kataka kuyakabili Maisha.

# HABARI PICHA














**Picha zote ni tukio la uzinduzi wa kitabu cha EDWARD MORINGE SOKOINE MAISHA NA UONGOZI WAKE**

TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## TUMEANUA MATANGA

Kama kulia tumelia
Huzuni kuhuzunia
Hatuna budi kutulia
Kumshukuru Jalia

Yote ni yake Jalia
Maisha kujitwalia
Letu ni kumsifia
Na si kumchukia

Kwani ni alopangia
Tangu kuumbwa dunia
Kiumbeche kumrudia
Kwa jinsi usofikiria

Mikono twakuinulia
Asante kuasentia
Shukrani kushukuria
Mipangoyo kutimia

Tumenyamaza kulia
Yajayo twayagangia
Maisha kufurahia
Ni budi iso halia

Tumtukuze Jalia
Mwisho kuufiki
Wemawe ukitimia
Ndo hivyo taishia

Matanga tunaanua
Msiba kutamatia
Kurasa twafunikia
Kwaheri twakutakia.

**Na. Amata Ric**
**Dar es salaam**

**Pumzika kwa amani Rey Stanley!**

## MWATEKA MWAMTEKEA NANI?

Swali tunajiuliza, wa kutujibu hakuna
Sijui mnatubeza, au maana hatuna
Ndugu tunawapoteza, lakini namna hatuna
Mwateka mwamtekea nani?

Watu vilio walia, ndugu zao walilia
Wadai wamepotea, polisi wawalilia
Twambieni tatulia, wa kwapi twaolilia
Mwateka mwamtekea nani?

Si walifu si wabaya, nyumbani mwawachukua
Mwayafanya pasi haya, ndo mana mwachukiwa
Hebu tuyajadili haya, na hatua kuchukua
Mwateka mwamtekea nani?

Nini kiini chake, utekaji Tanzania
Nani anafanya yake, mashakani kututia
Mana si kwa hiari yake, polisi tunahofia
Mwateka mwamtekea nani?


Sasa tunaogopana, maisha kama wanyama
Mapenzi siasa bayana, twawindwa kama wanyama
Ni kipi tunafichana, yawekeni wazi mapema
Mwateka mwamtekea nani?

Tunahitaji amani, tunahitaji utulivu
Maisha yana thamani, kamwe hayana utibivu
Bado tuna imani, na serikali sikivu
Mwateka mwamtekea nani?

Fungueni ndimi zenu, enyi wenye dhamana
Tujuzeni ndugu zenu, tusibaki tazamana
Hii ni kazi yenu, uhai kwetu amana
Mwateka mwamtekea nani?

**Jolita Msakuzi**
**Nachingwea - Lindi**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**




# OPERESHENI KASHMIR

Sasa Kinapatikana
kwa Tsh

**15,000/=**

Jikamatie

Nakala Yako

DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya
Riwaya
Kinondoni Morocco

Simu:
0655428085

Zammira

# KUTOKA MAKTABA: MAISHA NI MAPAMBANO—3

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka. (imerudiwa)**

SURA YA PILI

## TAMAA YA UTAJIRI WA HARAKA HARAKA

Mpepo, baada ya kusimulia juu ya mkasa wa maisha yake, ambayo yalijaa visa na mikasa alieleza jinsi alivyokumbwa na wimbi la utajiri wa haraka haraka.

Siku moja, majira ya mchana, Luzolo rafiki yake, alifika nyumbani kwake kumshawishi:

**Luzolo:** Ndugu Mpepo sahiba yangu, nina jambo ambalo ningependa kukwambia.

**Mpepo:** Niambie kwanza, huna haja ya kuniarifu. Wewe ndiyo mimi na mimi ndiyo wewe nadhani unafahamu hivyo.

**Luzolo:** Kweli kabisa. Habari yenyewe inahusu kujinasua na ufukara. Nimepata mawazo mapya kuhusu jam bo hili.

**Mpepo:** Sema tu rafiki yangu, ni ha bari njema zipi hizo.

Baada ya hapo Luzolo alimweleza rafiki yake kwa kirefu kuhusu mipango yake. Mipango ilihusu uchimbaji wa madini mkoani Rukwa. Alimwambia kwamba vijana wengi wametajirika sana kwa kazi hiyo: wengine wana maduka makubwa, mabasi ya abiria, mashine za kusaga nafaka na hata kufanya biashara na nchi za nje kwa kutumia makontena!

Mpepo kusikia hivyo, alivutiwa sana na kuanza kumdadisi mbinu watakazotumia hadi kufika huko na kuanza kazi ya uchimbaji madini.

**Mpepo:** Je, hakuna matatizo? Kwanza vifaa tutapata wapi?

**Luzolo:** Hakuna tabu. Tutapanda magari ya kawaida. Kwanza pale Mkuze sehemu yenye madini ni karibu na Tundu ma. Pia kuna watu ni naowafahamu. Vifaa vya kuchimbia ni sururu, jem be, sepetu na karai la ku zolea mchanga.

**Mpepo:** Kama nilivyosema hapo awali kweli hizi ni habari njema. Hata mimi nilikuwa sipati usingizi kwa kubakia katika hali hii. Ni kweli kabisa watu wengi wamepi ga hatua. Baadhi yao ni wa tumishi wa serikalini, katika mashirika, makampuni na hata wale wasiofahamika shughuli zao ni nini wanaishi maisha matukufu. Nadhani hakuna haja ya kupoteza muda; wazo tayari, iliyobaki ni utekelezaji. Si unajua usemi kwamba 'Ajizi nyumba ya njaa!'

**Luzolo:** Tuondoke kesho au kesho kutwa inafaa zaidi?

**Mpepo:** Bila shaka.

**Luzolo:** Haya mimi naondoka. Keshokutwa Jumamosi tutaondoka. Kama hatuku patwa na mkasa wowote tutafika Tunduma Jumapili saa za alasiri; hatimaye Mkuze.

**Mpepo:** Tunduma siyo Zambia? Naogopa kuvuka mipaka ya nchi, hasa nikikumbuka mateso ya siku za nyuma.

**Luzolo:** Sawa, Tunduma ni Zambia vile vile ni Tanzania—ina pande mbili kama vile Mli ma Kilimanjaro au Namang a kule Arusha.

**Mpepo:** Kama ni hivyo sawa. Juma mosi saa kumi na mbili alfajiri nitakuwa mlangoni.

Siku ya Jumamosi iliwadia. Mpepo aliamka mapema sana. Akamwamsha Sofi, mke wake. Kabla hajamweleza lolote Tabu akaanza kulia—maana hajazoea kuachwa peke yake kitandani majira kama yale. Hivyo Sofi akabaki kitandani amelala huku akimkumbatia Tabu. Sofi akamuuliza Mpepo.

**Sofi:** Kwani unataka kuniambia nini usiku wote huu?

**Mpepo:** Sina muda. Nina safari ya kwenda Rukwa na Luzolo. Tunakwenda kutafuta mali. Nadhani ulimwona jana hapa na tulikaa faragha kwa muda.

***Sehemu ya 4 itakujia toleo lijalo...***

# UFAHAMU UGONJWA WA MONKEY POX 'MPOX'

Mpox (awali ulijulikana kama Monkeypox) ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na virusi vya monkeypox, ambao umeendelea kuenea mwaka 2024 katika maeneo mbalimbali. Ugonjwa huu unahusishwa na makundi mawili ya virusi: Clade I na Clade II, huku milipuko mingi ikiripotiwa Afrika na baadhi ya kesi zikitokea Ulaya, Marekani, na Asia. Mpox huenea kupitia mgusano wa karibu na vidonda, majimaji ya mwili, au matone ya hewa kutoka kwa mtu aliyeambukizwa.

Kati ya mwaka 2023 na 2024, nchi kama Rwanda, Uganda, na Côte d'Ivoire ziliripoti kesi mpya za mpox, mara nyingi kutokana na safari za kutoka maeneo jirani. Wataalamu wa afya wanasihi umma kuwa makini, hasa kwa wale walio katika makundi yenye hatari kubwa, au wale wanaosafiri kwenda maeneo yenye milipuko ya ugonjwa huu..

Ni muhimu kupata habari kutoka kwa mamlaka za afya za eneo lako, kuepuka mgusano na walioambukizwa, na kufikiria chanjo ikiwa upo kwenye kundi lililo katika hatari.

## 2. Dalili zake ni zipi?

Dalili za mpox zinaweza kujitokeza kwa hatua kadhaa na mara nyingi huanza kwa dalili za jumla kabla ya upele kuonekana. Dalili hizo ni:

1. Homa ya ghafla.

2. Maumivu ya kichwa.

3. Kuvimba kwa tezi (hasa tezi za shingoni, kwapani, na kwenye kinena).

4. Maumivu ya misuli

5. Uchovu

6. Upele unaoweza kuanza usoni na kisha kuenea kwenye sehemu nyingine za mwili kama mikono, miguu, na hata kwenye sehemu za siri. Upele huu huanza kama madoa mekundu au makovu na baadaye huwa na majimaji au usaha.

Dalili hizi zinaweza kudumu kwa wiki mbili hadi nne, na wakati mwingine, zinaweza kuwa kali zaidi kwa watu wenye kinga dhaifu ya mwili au hali za kiafya zilizopo kabla.

## 3.Ugonjwa huu unasqbabisha kifo?

Mpox kwa kawaida si ugonjwa unaosababisha vifo vingi, lakini katika hali fulani, unaweza kusababisha vifo hasa kwa watu wenye kinga dhaifu au watoto wadogo. Kiwango cha vifo kinatofautiana kulingana na aina ya virusi (clade) vinavyosababisha ugonjwa huo. Kwa mfano, Clade I (ambayo huonekana zaidi Afrika ya Kati) ina kiwango cha juu cha vifo ikilinganishwa na Clade II (inayoenea zaidi Afrika Magharibi na sehemu zingine). Kiwango cha vifo cha Clade I kinaweza kufikia hadi asilimia 10 katika baadhi ya milipuko, wakati Clade II ina kiwango cha chini zaidi, karibu asilimia 1.

Kesi za vifo hutokea zaidi kwa wagonjwa walio na hali nyingine za kiafya kama vile UKIMWI, pamoja na wale wanaopata huduma duni za afya.

## 4. Nchi zilizoathirika zaidi Afrika

Nchi kadhaa za Afrika zimeathirika sana na mlipuko wa Mpox, hasa zile zilizo na kiwango kikubwa cha mawasiliano na wanyama walio na virusi au maeneo yenye milipuko ya virusi vya Clade I. Baadhi ya nchi ambazo zimeathirika zaidi ni:

1. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) – Imeathirika zaidi kutokana na uwepo wa Clade I, na milipuko ya Mpox imekuwa ikiendelea kwa miaka kadhaa.

2. Nigeria – Hii ni moja ya nchi zilizoathirika zaidi na Clade IIa, huku ikiwa na visa vingi vilivyoripotiwa tangu 2017.

3. Cameroon – Inaripotiwa kuwa na visa vya Clade I na Clade IIa.

4. Ivory Coast (Côte d'Ivoire) – Imeripotiwa kuathirika na mpox katika baadhi ya maeneo ya nchi.

5. Sudan ya Kusini – Imekuwa na visa kadhaa vya ugonjwa huu, hasa kutokana na ukosefu wa miundombinu ya afya inayofaa.

Nchi nyinginezo kama Rwanda na Uganda pia zimeripoti visa vya mpox kwa mwaka 2024, na milipuko imehusishwa na safari za kimataifa au mgusano ya moja kwa moja na wanyama walioathirika.

## 5. Tahadhari za kuchukua

Ili kupunguza hatari ya kuambukizwa mpox, jamii inapaswa kuchukua tahadhari zifuatazo:

1. Epuka mgusano ya karibu na watu walio na dalili za mpox, hasa wale walio na upele au vidonda vya ngozi.

2. Tumia vifaa vya kujikinga kama glavu na barakoa unapo hudumia au kuwa karibu na mgonjwa wa mpox ili kuepuka kugusana moja kwa moja na majimaji ya mwili au vidonda.

3. Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji au tumia vitakasa mikono (sanitizer), hasa baada ya kugusa vifaa au sehemu ambazo zinaweza kuwa na virusi.

4. Epuka kugusana na wanyama walio katika hatari*ya kuwa na mpox, kama vile wanyama wa porini, kwani mpox inaweza kuambukizwa kutoka kwa wanyama hadi kwa binadamu.

5. Elimu kwa jamii kuhusu dalili za mpox na jinsi inavyosambaa, pamoja na kuhimiza watu kujitenga na kuomba matibabu mapema wakiona dalili za ugonjwa huu.

6. Watu walio katika hatari kubwa (kama wafanyakazi wa afya au wale wanaoshughulika na wanyama) wanashauriwa kufikiria kupata chanjo ya mpox ikiwa inapatikana katika eneo lao.

Hatua hizi zinaweza kusaidia kupunguza maambukizi katika jamii na kudhibiti mlipuko wa ugonjwa huu.

## 6. Tiba

Mpox haina tiba maalum, lakini kuna matibabu yanayoweza kusaidia kupunguza dalili na kupambana na maambukizi. Watu wengi wanaweza kupona bila dawa maalum, lakini matibabu yafuatayo yanaweza kutumika kusaidia hali ya mgonjwa:

1. Matibabu ya dalili – Homa, maumivu ya kichwa, na maumivu ya mwili yanaweza kutibiwa kwa dawa za kupunguza maumivu na homa kama vile paracetamol au ibuprofen.

2. Kinga na chanjo – Chanjo iliyoundwa kwa ajili ya ndui (smallpox), kama MVA-BN (Imvamune/Imvanex), imeonekana kuwa na ufanisi dhidi ya mpox. Chanjo hii inaweza kutolewa kwa wale walio kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa.

3. Ant virus – Dawa kama tecovirimat (TPOXX) inaweza kutumika kutibu mpox katika kesi kali, ingawa matumizi yake bado yanasimamiwa kwa uangalifu.

4. Huduma ya uangalizi wa karibu – Watu wenye mpox kali au wenye kinga dhaifu wanaweza kuhitaji kulazwa hospitalini kwa uangalizi wa karibu, hasa kwa wale walio na vidonda vikubwa au maambukizi mengine yanayoweza kutokea.

Wagonjwa walio na mpox wanashauriwa pia kupumzika, kunywa maji ya kutosha, na kuhakikisha wanapata lishe bora ili kusaidia mwili kupona.

**7. WHO wanasemaje**

Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema kwamba Mpox ni tishio kubwa la afya ya umma, na mwaka 2024 lilitangazwa kuwa dharura ya kiafya ya kimataifa. WHO imezindua mpango wa kimataifa wa kuimarisha maandalizi na mwitikio dhidi ya mlipuko huu. Mpango huu unalenga kudhibiti maambukizi ya mtu kwa mtu kwa kuimarisha ufuatiliaji, utafiti, na kuhakikisha usawa katika upatikanaji wa chanjo na matibabu.

***Imeandaliwa kwa msaada wa mtandao***

# RAIS WA CHUO – 03

**"Tumechelewa Ramin," alisema Balonzi kwa sauti ya chini iliyokata tamaa.**
**"Hatujachelewa ndiyo maana mwanzo nilikuuliza nani mwingine anajua hili ukasema hakuna zaidi yetu. Si ndio?"**

**Endelea…**

"Ndiyo."
"Hao watu, kwa sababu naamini wanataka kutoa rushwa kwa hao watu hamsini waliowahitaji hawatotaka kuonana nao watu hao. Watamtumia Hasheem kumaliza hili," alisema Ramin. Balonzi alisikiliza kwa makini.
"Kwa hiyo, wakati wao wanakamilisha misheni yao namna hiyo, nasi tunaanza misheni yetu. Hizo fedha wakizileta tunazichukua na kazi yao hatutaifanya." Ramin alitulia.
"Inawezekanaje?" Balonzi aliuliza.
"Very easy! Hii ni rushwa – kupokea au kutoa rushwa ni kosa kisheria. Hilo moja. Pili, wanaotekeleza mpango huu ni wazi sio wanachuo, ikibainika wamefanya hivyo ni aibu kwa Taifa. Ili kutotaka kuchafuka hawatofanya chochote," Ramin alifafanua.
"Nimekuelewa," Balonzi aliafiki.
"Hatujui mpango wao wa mwisho utakuwaje. Yumkini wanataka kutoa fedha kwa hao watu. Ikiwa hivyo, fedha zipokelewe tuzitumie lakini lengo letu liwe palepale. Kanyika akose urais kwa kutotosha kura upande wake sio wanavyotaka wao," alimaliza Ramin. Baada ya makubaliano waliagana.

❦

"Ni kweli hizi taarifa nizisikiazo?" Swali la kwanza la Nyambuna baada ya kukutana na Kanyika.
"Nilifikiria hivyo kabla ya kukutana na Kikoti." Jibu lililonyooka lilitoka kwa Kanyika. Nyambuna alimtazama usoni kama mama aliyemkagua mwanawe. Kwa umri wao, Kikoti alifaa kuwa uzao wa Nyambuna japo hakupenda kumwita mama. Alimwita shangazi kama alivyomwita Alvie na Thebby. Pengo la umri kati yao lilimfanya Kanyika kuhisi kama angalimdanganya basi alimdanganya mama yake. Kwa hofu ya dhambi ya kumdanganya mama, ukweli wake ulikuwa dawa tosha katika kidonda cha mama huyo.

"Ilikuwaje?" Nyambuna alirusha swali lingine.
"Shangazi, usiku huu. Ingefaa tusilizungumzie tena hili. Nilifikiria kujitoa kwa sababu ya kukosa sapoti. Hata hivyo, sasa si kitu. Nitapambana hadi mwisho," alisema Kanyika.
"Sapoti gani uliihitaji? Fedha, watu wa kukusaidia kampeni au nini?"
"Ni mlolongo mrefu shangazi. Naomba nikuhakikishie fikra hizo hazipo tena. Tumezungumza kwa kirefu na Kikoti. Tumekubaliana kupambana mpaka mwisho. Kura ziamue hatma yetu," Kanyika alijitetea.
"Ok! Nimekuelewa. Tambua kuwa, lipo kundi kubwa nyuma yako. Kundi hilo ni kama upepo uvumao – huwezi kuuona lakini utauhisi uwepo wake. Unaweza kudhani unapambana peke yako. Nakuhakikishia mwanangu, wapo wanaopita njia nyingine kuhakikisha unashinda," alisema Nyambuna.

Maneno hayo yalizunguka kwa haraka kichwani kwa Kanyika. Alimtazama Nyambuna kwa macho yaliyomwambia jambo – jambo ambalo halikuelezwa kwa maneno, bali moyo.
"Nashukuru shangazi," alisema Kanyika ilhali moyo wake ukisita kuzipokea baraka zile. Hakuwa na budi kukubali ingawa alijua kazi kubwa imeshafanywa upande wa pili. Kwisha zungumza naye kwa muda mchache, Nyambuna alimruhusu Kanyika aondoke akapumzishe akili kwa ajili kumalizia kampeni siku inayofuata. Kwa usiku ule, ilibakia siku moja ya kampeni, nayo ni siku iliyofuata ambayo. Kwa mujibu wa taratibu, ilikuwa siku ya mwisho ya kampeni kabla ya uchaguzi wenyewe siku ya mbele yake.

❦

Simu ya Kanyika iliita, alipoitazama kwenye kioo alishtuka. Alibetua mkono wake wa kuume kuangalia saa – ilikaribia saa mbili na dakika tano usiku. Aliitazama tena namba iliyompigia kabla hajakata shauri kuipokea. Maneno machache yalitosha ndani ya sekunde kadhaa. Maneno hayo yalimtaka kufika haraka alikohitajika wakati ule. Alikuwa Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Mjaka Chuma. Ghafla mwili wake ulitota kwa jasho ingawa kulikuwa na baridi. "Mambo haya yanakuwaje. Mara hii yameshafika mpaka kwa Makamu Mkuu wa

Chuo?" Alijiuliza. Wakati akitafakari juu ya simu ile mlango wa chumbani kwake ulifunguliwa kwa fujo.
"Uko tayari?" Kikoti aliuliza.
"Naam!" Kanyika aliitikia. Bila kupoteza tena muda waliondoka.

Wajihi wa Profesa Mjaka Chuma – Makamu Mkuu wa Chuo ulichukiza kwa kila mtu aliyewahi kukabiliana naye – iwe wanafunzi au hata wakufunzi. Mara nyingi hakuwa mwenye mzaha. Sura yake haikustahili kuwa katika nafasi aliyokuwa nayo. Pengine ilipasa awe Jenerali wa Jeshi au hata jambazi sugu. Kila mara alikasirika bila sababu. Kanyika na Kikoti walipofika aliwaongoza kwenye ukumbi mdogo wa mikutano. Walipoingia huko waliwakuta watu wengine wanne; Shafi Kituka, Jonta Nyamwaro, Christopher James na Mpendae Rajabu.
"Kanyika!" Aliita Profesa Mjaka Chuma baada ya kuhakikisha kila mmoja aliketi mahala pake.
"Naam Profesa!" Kanyika aliitika kwa unyenyekevu.
"Bila shaka unafahamu kilichotokea?" Profesa Mjaka Chuma aliuliza.
"Nimesikia na Kituka alinipigia simu kuniarifu juu ya hilo. Lakini, nikuhakikishie Profesa, I have nothing to do with it," alisema Kanyika. Profesa Mjaka Chuma aliinamisha kichwa chini. Alitafakari kwa sekunde chache kisha alikiinua kumtazama kila mmoja. Baadaye aliuliza, "Inawezekanaje usijue?"
"Kwa sababu sijaratibu jambo hilo na sikuwahi kufikiria kuliratibu," Kanyika alijibu kwa utulivu.



MAKOLEKO KALIBONGE

o

Mandhari waliyokuwamo wakati huo yalisadifiana na utulivu wake. Kama hapakuwa na jambo kubwa upande au halikupa uzito mkubwa jambo hilo. Tofauti na watu wengine.
"Sawa. Hujaliratibu lakini waliofanya fujo ni watu wako," alisema Profesa Mjaka Chuma. Ithibati katika maneno yake ilikuwa kubwa. Macho yake yaliyobebwa kwenye kichwa cha duara yalimuangalia Kanyika bila kupepesa.
"Sidhani kama nina watu au nilikuwa na watu wanaoweza kufanya jambo la ovyo kama lile. Ndiyo maana nimesema sijaratibu na sikufikiria kuliratibu," alieleza Kanyika kwa kujiamini.

"Kanyika, we' ni mtoto mdogo sana. Hudhani kuwa unashindwa kutumia mbinu faafu kunidanganya mtu kama mimi. Profesa?" Profesa Mjaka Chuma alipaza sauti. Ukali wa sauti yake uliambatana na kishindo kikubwa juu ya meza. Ni mkono wake mzito ulitua juu ya meza ukaibamiza mbaa! Kanyika alitazama chini jasho likimvuja. Alihisi kitu. Kabla hajawaza ni kitu gani hicho Profesa Mjaka Chuma aliendelea, "Miongoni mwa watu waliohusika kufanya fujo ni pamoja na huyu…" alimnyooshea kidole Mpendae ambaye wakati wote alijikunyata kwenye kiti kilichopo kwenye kona ya meza. Kanyika aligeuka kumtazama Mpendae lakini macho yao yaliumana kwa sekunde moja tu kabla Mpendae hajageuka haraka.
"Ni yeye aliyesema nimewatuma kufanya fujo?" Kanyika aliuliza kitoto.
"We' hebu tuambie ilikuwaje," aliamuru Profesa Mjaka Chuma badala ya kujibu swali la Kanyika. Mpendae alianza kuelezea.
"Kanyika ndiye aliniagiza kufanya fujo," alianza kusema Mpendae. Kichwa chini akaendelea, "Tulikutana mara kadhaa akaniambia nihakikishe natumia mbinu zozote ninazozijua ili kuharibu taswira ya Kituka na Nyamwaro wasishinde kwenye uchaguzi huu. Hata leo tumekutana asubuhi akanisisitizia nifanye hivyo kwa kuwa ilikuwa siku ya mwisho. Aliniahidi akishinda urais atanichagua kuwa Mbunge." Mpendae alimaliza.

Si Kanyika tu hata Kikoti alishangaa kusikia habari hizo. Mpendae alieleza kitu ambacho kilikuwa kipya masikioni mwao. Alieleza mambo ambayo hayakuwemo vichwani mwao. Walitazamana kwa sekunde kisha kama waliambiana, kwa pamoja walimtazama Mpendae. Ni kama vile macho yao yalimsuta. Ni Mpendae huyu ambaye mara nyingi walikuwa naye katika kampeni lakini haikutokea hata fikra ya kumtuma kuratibu jambo kama hilo. Aliwaza Kanyika. Jambo baya zaidi aliposema aliahidiwa ubunge wa kuteuliwa. Alikumbuka namna alivyokutana naye asubuhi ya siku hiyo. Walikuwa njiani akitokea

# RAIS WA CHUO – 03

chumbani kwa mmoja wa waratibu wa kampeni siku hiyo. Hawakuzungumza jambo lolote zaidi ya salamu. Lakini hapo alidai wamezungumza akimsisitizia juu ya mpango wao. Yumkini ameahidiwa huo ubunge na Kituka. Aliwaza.
"Umesikia?" Waligutushwa na swali la Profesa Mjaka Chuma.
"Prof…" alisema Kikoti. Kabla hajaendelea alikatishwa.
"Kwa mujibu wa Students by laws, sasa hivi mlitakiwa muwe chini ya ulinzi mkali wa Polisi. Hili ni kosa. Mmeunda kikundi kisha mmeratibu kufanya vurugu. Kwa nini mfikie hatua hii? Kwa uchaguzi gani?"
Maswali mfululizo yalimtoka Profesa Mjaka Chuma. Sura yake ilibadilika kila dakika. Iliogofya zaidi. Aliendelea, "Hili ni kosa kubwa sana mlilolifanya. Nakuahidi halitaishia hapa."

Hofu, woga na simanzi zilitanda katika mioyo ya Kanyika na Kikoti. Kauli ya Profesa Mjaka Chuma kwamba hilo jambo halitoishia hapo ni kauli mbaya kuwahi kupenya kwenye ngoma za masikio yao. Haikosi adhabu yao ni kufukuzwa Chuo.
"Profesa nakuomba lisifikie hatua hiyo." Hatimaye Shafi Kituka alisema baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu.
"Imethibitika, kwa mujibu wa Mpendae, kuwa ni wao waliofanya fujo. Kwa hivi, naomba hili jambo liishie kwako. Binafsi, nimewasamehe as long as leo ilikuwa siku ya mwisho. Kwa hiyo tulimalize tu hapa," alisisitiza Kituka. Profesa Mjaka Chuma alinyamaza kimya akifikiri. Kisha aliinua kichwa kuwatazama kila mmoja kwa zamu – akianzia kwa Kanyika na kumalizia kwa Kituka, akasema, "Huu uchaguzi unafuatiliwa kwa karibu na vyombo vya usalama. Sitarajii kutokea kituko kingine cha ajabu."
"Tumekuelewa mkuu." Waliitikia kwa pamoja kisha walitawanyika.

❦

Kitendo cha kuitwa kwenye kikao na Makamu Mkuu wa Chuo hakikuwaumiza Kanyika na Kikoti. Bali kilichowaumiza moyo ni ajenda ya kikao hicho – kuratibu fujo kwenye mkutano wa mpinzani wake. Jambo hilo halikuwahi kufikiriwa si kwao tu bali hata kwa watu wao waliowaamini. Wakati fulani fikira zao ziliwaambia walisalitiana kila mmoja kwa nafasi yake. Walakini, kwa sababu zipi hasa? Wakati mwingine walifikiria labda watu wao wa karibu hasa Hasheem huenda aliratibu.
"Inawezekana vipi?" Alijiuliza Kanyika.
Ilikuwa hivi; siku hiyo ya mwisho wa kampeni, Kanyika na Kikoti walianzia kampeni kwenye Chuo cha Sayansi ya Jamii ambako ni uwanja wa nyumbani wa Kituka kama walivyoita wenyewe. Kisha walitakiwa kumalizia Chuo cha Elimu, kama ilivyoelekeza ratiba yao. Na, kwa upande wa Kituka ilikuwa kinyume chake. Baada ya kumaliza kampeni Chuo cha Sayansi ya Jamii walikwenda Chuo cha Elimu ambako wakiwa katikati ya kampeni, Kanyika alipokea simu ya Kituka kumtaarifu kuwa kundi la watu aliosema wametumwa lilianzisha fujo. Watu hao walidhibitiwa na watu wa Kituka kisha waliripoti tukio hilo kwa Makamu Mkuu wa Chuo – Profesa Mjaka Chuma.

Taarifa hiyo haikuelezwa kwamba miongoni mwa watu waliofanya fujo ni Mpendae Rajabu. Aliichukulia kawaida tu. Japo alimwomba radhi wakati huo hakudhani kama litakuwa kama lilivyotokea. Baada ya kampeni ya siku hiyo alikutana na Kikoti pamoja na Hasheem. Kila mmoja alikana kujihusisha na tukio hilo. Waliafikiana kulichunguza japo halikuwa na maana yoyote baada ya uchaguzi. Bali walitaka kujiridhisha. Walipofikia muafaka wa kulichunguza walitawanyika. Usiku ndipo walipigiwa simu kuitwa kwenye kikao na Makamu Mkuu wa Chuo.
Jambo lingine lililomsikitisha Kanyika, ni kwamba katika mkutano ule, timu ya upande wa pili ilikuwa na watu wote wa juu. Ilikuwaje wao waitwe wawili tu? Alijiuliza. Kwa hiyo, aliamini kuna mchezo ulichezwa.

❦

SIKU YA UCHAGUZI
Kulipopambazuka, ilikuwa siku iliyosubiriwa kwa muda mrefu – siku ya uchaguzi. Siku hiyo ilikuwa ndiyo fainali ya mchuano wa wiki mbili za kumwaga sera, kuchafuana, kujisifia na kujinadi. Kilichosubiriwa ni kupiga kura kisha zihesabiwe na baadaye atangazwe mshindi. Mshindi huyo ndiyeataunda serikali ya wanafunzi ambayo itahudumu kwa mwaka mmoja baadaye kabla ya kupisha mchakato mwingine kama huo.

Zoezi la kupiga kura lilipangwa kuanza majira ya saa mbili asubuhi hadi saa kumi alasiri. Kila mgombea wa nafasi zote – urais, ubunge, uwakilishi wa skuli na uongozi wa mabweni alikuwa na wakala wake ambaye alitakiwa kuhakikisha usalama wa kura zake. Baada ya ukaguzi wa vifaa – masanduku ya kuhifadhia kura, karatasi za kupigia kura na wasimamizi wake, zoezi la kupiga kura lilianza rasmi. Kila mwanafunzi alikuwa na haki ya kupiga kura kumchagua mtu aliyedhani atamtumikia kwa uadilifu. Siku hiyo ilianza kwa ishara nzuri kwa kila upande kulingana na maandalizi japo Kituka alikuwa na uhakika wa asilimia mia moja kuibuka na ushindi. Kwa hivi, baada ya kupiga kura aliwakusanya watu wake muhimu wakaingia katika moja ya madarasa. Wakatulia.

Kwa upande wake Kanyika, siku hii haikuwa muhimu kama zilivyokuwa siku nyingine. Jitihada zake katika kuwaongoza wanafunzi wenzake zilifika ukingoni. Kila alivyojaribu kupima matokeo alijiona amepoteza muda mwingi. Muda huo aliujutia akaona bora angeutumia kujiandaa zaidi kimasomo. Baada ya kupiga kura alirudi hostel akajifungia chumbani kwake. Kwa jinsi alivyohuzunika na siku hiyo aliamua kuzima simu. Hakutaka kuzungumza na mtu yeyote hadi matokeo yatakapotangazwa. Kabla ya kuzima simu alimpigia Kikoti kumtaarifu kuwa atakuwa chumbani siku hiyo hadi yakishatangazwa matokeo atatoka.
Kadiri muda ulivyokuwa unasogea ndivyo joto la matokeo lilivyozidi kupanda. Shauku ya wengi ilikuwa kufurahia ushindi wa waliomchagua. Hata hivyo, furaha yao haikutakiwa kuwa kikwazo cha kuendelea na kilichowapeleka chuoni. Walioshinda waliruhusiwa kufurahi. Mwisho wa furaha yao ni kuendelea na masomo. Kadhalika, walioshindwa waliruhusiwa kuhuzunika. Nao mwisho wa huzuni yao ni kuendelea na masomo.

Ilipotimu saa kumi alasiri zoezi la kupiga kura lilifungwa. Zoezi lililofuata lilikuwa kuhesabu kura hizo. Wakala wa kila mgombea alikuwa makini kuhakikisha hesabu zinakwenda sawa. Kufikia saa kumi na mbili matokeo ya wabunge, wawakilishi wa skuli na viongozi wa mabweni yalikwishabandikwa kwenye mbao za matangazo. Matokeo ya Urais yaliendelea kuhesabiwa.

❦

Mlango wa chumba cha Aikael Kanyika uligongwa kwa fujo. Kanyika alishtuka kutoka usingizini. Alijikokota kivivu hadi mlangoni akaufungua.

“We’ una shida gani? Hupatikani kwenye simu.” Alikuwa Kikoti.
“Sikutaka usumbufu,” alijibu Kanyika kwa sauti iliyojaa usingizi.
“Usumbufu wa nini?” Kikoti aliuliza. Alikwishaingia chumbani kwa Kanyika. Moja kwa moja akaketi juu ya meza. Akasema, “Unahitajika. Matokeo yapo tayari na hayawezi kutangazwa bila uwepo wako.” Maneno ya Kikoti yalimwingia Kanyika tumboni badala ya ubongoni. Tumbo lilivurugika akahisi kuharisha. Jasho likamtoka na mapigo ya moyo yalimwenda kasi ajabu.

Dakika moja ilipita akiwaza afanye kitu gani. Akubali kwenda au akatae. Kichwani aliiwazia idhilali itakayomkabili baada ya matokeo kutangazwa. Alijua kama amepata kura nyingi basi hazitozidi kumi na tano. Vinginevyo ni aibu tupu. Kama ndivyo, kuna haja gani ya kwenda? Kwenda kumshuhudia Kituka akishangilia ushindi wa kishindo? Hapana. Aliwaza. Hata hivyo, alilazimika kwenda. Taratibu zilimtaka awepo wakati wa kutangazwa matokeo bila kujali ameshinda au ameshindwa.

“Kanyika, vipi?” Alishtushwa na Kikoti ambaye wakati wote alitulia akimuangalia namna alivyobutaika.
“Ok! Wacha nijiandae,” alisema Kanyika.
Baada ya kujiandaa walitoka. Moja kwa moja hadi kwenye ukumbi ambao ulipangwa kwa ajili ya tukio hilo. Wanafunzi walikuwa wengi mno nje ya ukumbi. Walifurahi sana. Kwa jinsi walivyofurahi ni kama vile wote walimpigia kura mgombea mmoja. Wote walifurahi. Moyo wa Kanyika ulipiga kite kwa hofu ya kudhalilika. Mbali na wanafunzi hao pia walikuwepo Polisi waliozunguka ukumbi. Polisi hao walikuwa na silaha. Walikuwa tayari kudhibiti aina yoyote ya fujo itakayotokea baada ya mshindi kutangazwa.
Ndani ya ukumbi hali ilikuwa tofauti na nje. Haukujaa na ulizizima kwa kimya cha kaburini. Watu wachache waliruhusiwa kuingia.

***Haya kumekucha… nini kitajiri? Tukutane toleo lijalo***

# Tangazo




www.richardmwambe.com

JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com